**Miili** iliyoopolewa ajali ya boti Ziwa Victoria yafikia 9

UKURASA 2

**Polisi** yanasa mtandao wa watuhumiwa wa mauaji

UKURASA 3

RIPOTI MAALUMU

**Mama** asimulia alivyomwokoa mtoto mikononi mwa mganga jadi

UKURASA 4



MWENDO WA KAPELO

UKURASA 13


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Septemba 29, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581814


www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz  www.facebook.com/nipashetz  www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Samia: Sijawahi kuua mtu, labda sisimizi

• **Ataka** UWT kujibu mapigo ya wapinzani, amaliza ziara Ruvuma kwa kishindo... *Endelea Ukurasa 2*



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akipokea zawadi ya picha yake ya kuchorwa kutoka kwa Makamu Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa Tanzania (UWT) Taifa, Zainab Khamis Shomari, kabla ya kufunga Kikao Maalum cha Baraza Kuu la UWT, wilayani Songea, mkoani Ruvuma, jana. **PICHA: IKULU**

## Sindano, pedi, nguo zaokotwa ufukweni mwa Bahari ya Hindi

UKURASA 3



## Mwili askari wakutwa msituni baada ya kupotea kwa siku 50

UKURASA 3

**MICHEZO** YANGA VITANI DAR, SIMBA DODOMA UK.24 | **MAONI, KATUNI** UK.6

# Miili iliyoopolewa ajali ya boti yafikia tisa

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MIILI ya watu saba imeopolewa katika Ziwa Victoria na kufanya idadi kufikia tisa baada ya ajali ya boti ya mizigo ya MV. Sea Falcon.

Boti hiyo ilikuwa na zaidi ya abiria 30 ikitokea Kirumba mkoani Mwanza kwenda kisiwani Goziba, kilichoko mkoani Kagera.

Ajali hiyo ya boti lenye usajili namba MTZ 012212 ilitokea juzi Septemba 25 mwaka huu, saa 12:00 asubuhi katika Ziwa Victoria kilometa mbili kutoka nchi kavu ya mwalo wa Bwiru ulioko wilayani Ilemela, mkoani Mwanza.

Akizungumza jana wakati wa uopoaji wa miili hiyo, Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Wilaya ya Ilemela ambaye pia ni Kaimu Kamanda Mkoa wa Mwanza, Mrakibu Msaidizi (ASF) Deusidedith Ruta, alisema mwili wa pili uliopolewa juzi majira ya jioni.

"Leo jana) tumeopoa miili saba na kufanya idadi kufikia tisa na miili yote ni ya jinsia ya kiume. Kati ya miili hii, miwili pekee ndiyo imetambuliwa na ndugu," alisema Ruta.

Alisema miili yote imepelekwa katika Hospitali ya Rufani Mkoa wa Mwanza (Sekou Toure) na kuwa shughuli ya utafutaji katika eneo la tukio bado inaendelea kutokana na kutokuwapo kwa idadi rasmi ya watu waliopanda boti hiyo.

Alisema baadhi ya miili ilipatikana katika eneo ilikozama boti hiyo, huku mingine ikipatikana katika maeneo mbalimbali ya fukwe za Ziwa Victoria.

"Kutokana na hali hiyo, niwaombe viongozi wa wavuvi pamoja na wavuvi pindi watakapoona miili ikielea wasisite kutoa taarifa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ili kuifikisha katika maeneo rasmi.

"Niwatake ndugu wanaohisi kuwa walikuwa na ndugu zao katika boti hili kuhakikisha wanafika katika hospitaliya Sekou Toure ili kutambua ndugu zao," alisema Ruta.

Akizungumza katika eneo la tukio, shuhuda wa tukio hilo ambaye pia ni mmiliki wa eneo la mwalo walipokuwa wakipokewa majeruhi hao pamoja na miili iliyoopolewa, Joseph Masole, alisema mtu wa kwanza kuwapatia taarifa hiyo alikuwa miongoni mwa manusura wa ajali hiyo.

"Alifika akasema tupo watu kama 60, tunahitaji msaada nikatuma mitumbwi ikaenda kuokoa watu na wakati huo tukiendelea na kuomba msaada kutoka vyombo vya ulinzi na usalama ambako gari za wagonjwa zililetwa kwa ajili ya kuwapokea wote waliokuwa wakiokolewa," alisema Masole.

Kamanda wa Polisi Mkoa Mkoa wa Mwanza, Naibu Kamishna (DCP) Wilbroad Mutafungwa, alithibitisha kuwakamata watu watatu akiwamo mmiliki wa boti hiyo, Amon Lutabanzibwa, kutokana na kutumia boti hiyo kubeba abiria bila kuwa na kibali cha kufanya kazi hiyo kutoka Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC).

"Miili minne tayari imetambulika na kukabidhiwa kwa ndugu ambako serikali kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza imetoa majeneza, Sh. 100,000 kwa kila familia pamoja na kugharamia usafirishaji wa miili," alisema DCP Mutafungwa.

Mkurugenzi wa Huduma za Udhibiti kutoka TASAC, Leticia Mutaki, alisema leseni ya boti hiyo inataka kibebe watu wasiozidi watano, lakini wenyewe walibeba zaidi ya 30.

Kutoka na tukio hilo, Mutaki aliwataka wamiliki pamoja na wasafirishaji wa vyombo vya majini kuzingatia masharti ya leseni wanazopewa na matakwa ya leseni hizo.

"Leseni zimebainisha kabisa kwamba wewe kanuni yako ya kubeba mizigo ni kiasi kadhaa na kama ni abiria ni abiria kadhaa na kwa boti hii iliyokuwa na urefu wa mita 17 kiwango chake ilikuwa ni watu wasiozidi watano," alisema.



Wafanyabiashara wadogo maarufu machinga wakiwa wamepanga bidhaa zao, kwenye eneo la waenda kwa miguu katika Barabara ya Uhuru, Ilala Karume, jijini Dar es Salaam jana, kitendo kinachosababisha usumbufu kwa wapita njia. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Samia asema hajawahi kuua mtu

**Na Waandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema katika maisha yake hajawahi kuua mtu labda sisimizi, huku akiwataka wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuwajibu wale wote ambao wamekuwa wakimshambulia kwa maneno, ikiwamo kumwita muuaji.

Alitoa kauli hiyo jana wakati akihutubia wanachama wa chama hicho pamoja na viongozi wa serikali katika sherehe za kilele cha Baraza Kuu la Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT).

Rais Samia alisema amesikia maneno hayo na kwa masikitiko makubwa kwa namna anavyoshambuliwa kuwa yeye ni muuaji ilhali hajawahi kuua mtu.

"Sisimizi nimeua lakini mtu sijawahi, sijawahi kuua. Sasa ombi langu kwenu ni kusimama imara. Ukweli mnaujua mdomo wa Mwenyekiti mmoja kujibu hoja zile hauwezi, pengine mwenyekiti wakati mambo haya yanatokea ninakuwa katika majukumu mengine.

"Kwa hiyo msimame muwajibu. Ndugu zangu, mnahofia nini? Hakuna cha kuhofia hapa. Mkiambiwa Mwenyekiti na Rais wenu muuaji, waambieni kweli ameua nguvu za upinzani. Ameua njia zote za kuzidisha umaskini ndani ya nchi yetu, amekuza uchumi wa nchi hii na ameua mambo hasi ya kuturudisha nyuma,"alisema.

Rais Samia alisema kweli ameua giza lililokuwa limeigubika nchi na kwamba, sasa nchi inang'ara kimataifa na hayo ndiyo mambo ambayo ameua na si mtu.

Alisema wakati nchi ikielekea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu na Uchaguzi Mkuu mwakani, wanachama wa CCM wanapaswa kushikamana kuwa kitu kimoja ili kushinda kwa kishindo.

"Kamati za ushindi mnazoziweka hivi sasa lazima ziwe kwa ajili ya kukivusha chama na siyo watu, kwani haya mambo ndiyo yameturudisha nyuma kutokana na kuunda kamati za kuvusha watu, badala ya kuvusha chama," alisema Rais Samia.

Vilevile, alisema anafahamu hivi sasa watu tayari wameanza kujipanga kwa vitenge na fedha kwa ajili ya kutoa kwa wapigakura, lakini kinachopaswa kuzingatiwa ni kuwaunga mkono watu wenye sifa na siyo vinginevyo.

**CCM HAINA MBADALA**

Rais Samia alisema: "Tunapaswa kuunga mkono watu wenye sifa siyo kwa ushemeji au ukwe, kwani ninaamini CCM bado haijapata mbadala wa kuongoza nchi hii, hivyo tuwaunge mkono watu wenye sifa za kuongoza."

Kadhalika, alisema chama hicho kimefanya mabadiliko makubwa ikiwamo kuwaondoa viongozi ambao walikuwa wanakiuka maadili.

"Kuna viongozi ambao wao walikuwa wanakopa hawalipi. Kuna viongozi ambao wao ndio walikuwa wanajihusisha na kangomba, tumewaondoa na tunaendelea kuwapunguza wale ambao wanakiuka maadili.

"Sisi tunashirikiana na vyama vingine duniani, hivyo vinapaswa kuona namna tulivyo nyooka katika maadili," alisisitiza.

**AWAAGA KWA AINA YAKE**

Rais Samia ambaye amemaliza ziara yake ya siku nne mkoani Ruvuma, mara baada ya kuhutubia maelfu ya wananchi waliojitokeza katika uwanja wa Majimaji, aliamua kutembea huku akiwapungia mkono kisha baadaye kupanda katika gari na kuondoka.

Katika hotuba yake, Rais Samia aliagiza Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na serikali mkoa huo kuhakikisha wanapunguza uharibifu wa mazingira katika maeneo mbalimbali yenye matatizo.

Kuhusu barabara kutoka Songea-Makambako, alisema iko katika mchakato na serikali inafanya kila njia kuikarabati na ile kutoka Likuyufusi- Mkenda mpakani mwa Msumbiji na Tanzania, itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami kwa kilometa 60.

Kwa upande wa elimu, alisema kwa sababu shule ya Rais Samia Suluhu Hassan kuonesha mfano mzuri wa kutumia gesi, ameagiza shule nyingine pamoja na taasisi mbalimbali ziige mfano.

Awali, Mwenyekiti wa UWT, Mary Chatanda, akizungumza katika kilele cha Baraza Kuu UWT, alisema wamejipanga kuhakikisha CCM inashinda kwa kishindo uchaguzi zijazo.

"Sisi tayari tumeshaanza kuunda kamati za ushindi katika uchaguzi mkuu mwakani na ushindi ni lazima mitano tena kwa mwenyekiti wetu," alisema.

Alisema UWT inakemea tabia ya baadhi ya wanawake wa chama cha upinzani ambao hivi karibuni walimshambulia kwa kumwita muuaji.

"UWT inalaani kitendo cha wanawake hawa kumwita mwenyekiti wetu kuwa ni muuaji wakati wao ndiyo kipindi cha nyuma katika siku ya wanawake duniani walimwalika na kumpatia tuzo kwa kazi nzuri aliyoifanya hali hii haikubaliki na sisi tumechoka kuwavumilia," alisema Chatanda.

**IMEANDALIWA na Paul Mabeja (DODOMA) na Gidion Mwakanosya (RUVUMA)**

HABARI KITAIFA

# Polisi yanasa mtandao watuhumiwa wa mauaji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

JESHI la Polisi Mkoa wa Dodoma limekamata genge la watu wanne wanaotuhumiwa kuhusika na matukio manne ya mauaji yaliyotokea hivi karibuni jijini hapa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, George Katabazi, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari na kuwataja watuhumiwa hao kuwa ni Paulo Daudi Mwaluko (22), Isack Richard (24), Erest Richard (18) na Silvanus Shotoo (21), wote wakazi wa Mtumba jijini hapa.

Kamnda Katabazi alisema watuhumiwa hao wanadaiwa kuhusika katika tukio la Julai Mosi, mwaka huu, katika eneo la Mahomanyika, Nzuguni la mauaji ya mabinti wawili ndani ya glosari waliyokuwa wakifanya kazi kisha miili yao kuchomwa moto.

Alisema tukio la pili lilitokea Agosti 28 mwaka huu, eneo la Mbuyuni Kizota ambako aliuawa Michael Richard (36), mke wake na watoto wao watatu waliojeruhiwa na kufungwa katika godoro walilolalia kisha kuchomwa moto ili waungue.

"Tukio la tatu ni ambalo limetokea Septemba 6, mwaka huu, eneo la Mkonze ambapo mama mmoja na mtoto wake waliuawa, tukio la nne lilitokea Septemba 16 mwaka huu, huko katika Mtaa wa Segu Bwawani Nala ambapo mabinti watatu waliuawa na kuchomwa moto na mama mwenye nyumba kujeruhiwa," alisema.

Katika tukio la Nala, waliuawa Milcah Robert (12) aliyehitimu darasa la saba Shule ya Msingi Chihoni, Fatuma Mohamed (20), dada wa kazi, Makiwa Abdallah (16) huku Mama Lusajo Mwasonge (40) akijeruhiwa. Tukio la Mkonze Mama Mwamvita Mwakibasi (33) na mtoto wake Salma Ramadhan (13) waliouawa.

Kamanda Katabazi alisema uchunguzi umebaini kuwa katika matukio yote hayo watuhumiwa walikuwa wakishapiga kwa kitu kizito wanaowakuta katika nyumba walizovamia huwafanyia vitendo vya udhalilishaji na kuwachoma moto ili ionekane ni hitilafu ya umeme imetokea.

"Uchunguzi zaidi unakamilishwa ili hatua zingine za kisheria zifuate, hivyo Jeshi la Polisi Mkoa wa Dodoma linawashukuru wananchi kwa ushirikiano wao uliofanikisha kukamatwa kwa mtandao huu wa mauaji," alisema.

# Mwili askari wakutwa msituni baada ya kupotea kwa siku 50

**Na Romana Mallya**

ASKARI wa kikosi cha Valantia (KVZ) Makao Makuu Mtoni, Zanzibar, Sajini Haji Machano Mohamedi, ambaye alitoweka kambini kwa siku 50 wakati wa mazoezi, mwili wake umekutwa msituni ukiwa umeharibika.

Askari huyo alitoweka kambini tangu Agosti 8, mwaka huu, na taarifa ilitolewa katika Kituo cha Polisi Dunga, Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja siku iliyofuata.

Taarifa iliyotolewa jana na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kusini Unguja, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Daniel Shillah, ilisema askari huyo alikuwa akihudhuria mafunzo ya uongozi katika chuo cha uongozi Jeshi la Kujenga Uchumi Dunga.

"Agosti 8, mwaka huu, majira ya saa 8:00 mchana katika msitu ulioko karibu na chuo hicho, askari huyo akiwa na wenzake katika mafunzo alipotea katika mazingira ambayo hayakueleweka.

"Baada ya wenzake kurejea kambini ndipo alipobainika alikuwa haonekani ndipo taarifa hizo zilipelekwa polisi na uchunguzi kuendelea," alisema SACP Shillah.

Alisema Septemba 26, mwaka huu, saa 10:00 alasiri kwenye msitu ulioko karibu na kambi ya chuo hicho, ulionekana mwili wa binadamu ukiwa umeharibika vibaya.

"Uchunguzi wa awali uliofanywa na Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali ulibaini mwili huo ukiwa na nguo na viatu ambavyo zinafanana na zile alizovaa askari huyo siku aliyopotea," alisema.

SACP Shillah alisema katika mfuko wa suruali aliyokuwa amevaa askari huyo ilipatikana simu ambayo imetambulia kuwa ni yake aliyokuwa akiitumia.

Alisema uchunguzi zaidi wa tukio hilo unaendelea ukiwamo Ulinganisho wa Vinasaba (DNA) kwa madhumuni ya kubaini ni kitu gani



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Kisutu, wakifanya usafi katika ufukwe wa Bahari ya Hindi, eneo la daraja la Selander kwa kushirikiana na taasisi ya Sanamare, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA:ENOCK CHARLES**

# Sindano, pedi zaokotwa ufukweni mwa bahari

**Na Enock Charles**

WADAU wa mazingira nchini waliojitokeza kusafisha ufukwe wa Bahari ya Hindi, wamekutana na sindano za hospitalini, pedi, plastiki za aina mbalimbali na nguo.

Kutokana na hali hiyo, wameitaka jamii kujenga utamaduni wa kulinda fukwe hizo na viumbe hai vilivyoko baharini na kuepuka mlipuko wa magonjwa unaoweza kutokea kutokana na uchafu.

Katibu wa Mipango wa Taasisi ya Sanamare, Pius Mollel, aliyasema hayo jana wakati wa zoezi la usafi katika fukwe hizo lililoshirikisha taasisi mbalimbali za mazingira na Shule ya Sekondari Kisutu waliosafisha ufukwe wa Selander Bridge, jijini Dar es Salaam.

Mollel alisema hali ya usafi katika fukwe walizotembelea jijini humo sio nzuri na kuomba wadau kuungana kuzisafisha mara kwa mara na kuzitunza.

"Leo tumekusanya taka mifuko zaidi ya 150 ambazo ni mchanganyiko wa vitu mbalimbali kama vile za hospitalini ikiwamo sindano, pedi za watoto, plastiki za aina mbalimbali na nguo za aina mbalimbali, vitu ambavyo havitakiwi katika fukwe zetu.

"Lakini hatujaishia hapo pia, tunachukua taarifa ya aina ya taka zinazopatikana hapa kwa wingi na chapa zilizoongoza kwa uchafuzi wa taka. Hii inasaidia kujua chanzo cha taka zinazopatikana ambazo tutazipeleka kwa mamlaka husika ili hatua mbalimbali zichukuliwe, " alisema.

Alipendekeza wahusika watakaopatikana kuwa bidhaa zao zinaongoza kwa kuzalisha taka hizo, wawajibike ili kupunguza athari katika fukwe nchini.

Pia alipendekeza kuanzisha mipango ya kurejeleza taka hizo (recycling) au kutoa fedha kwa mashirika ya kufanya usafi wa mazingira ili kuzipunguza.

Mwalimu wa Mazingira wa Shule ya Sekondari Kisutu, Anaely Mwakyeja, alisema kuna umuhimu wa elimu ya mazingira kutolewa kwa vijana katika shule za msingi na sekondari ili kujenga kizazi kinachojali mazingira kwa miaka ijayo.

"Tatizo hili la uchafu katika fukwe zetu pamoja na mambo mengine, linatokana na tabia binafsi za watu na kukosa uelewa wa elimu ya mazingira sasa tukiwafundisha wanafunzi kama hivi, tutajenga kizazi kilichostaarabika na kuheshimu mazingira.

"Kwa taka hizi kuna uwezekano wa kudhuru binadamu na wanyama hasa viumbehai wanaoishi ndani ya bahari mfano, humu tumekuta sindano, pengine ni za vijana wanaotumia madawa ya kulevya na wanazitupa tu kwa sababu hawajui umuhimu wa Bahari," alisema.

Mwalimu huyo pia, aliziomba mamlaka za serikali za mitaa kuzisimamia fukwe zilizoko katika maeneo yao kwa kuandaa siku maalum za usafi na kuhamasisha wananchi kuzipenda fukwe hizo kwa kuzifanyia usafi kila wakati.

"Fukwe nyingi zina serikali yake ya mtaa ninatamani sana zihamasishe jamii kuungana pamoja na hizi taasisi tofauti kuratibu kila mwezi kuwa na usafi kama huu wa leo," alisema.

Alisema kwa kufanya hivyo itakuwa ni njia rahisi kufanya bahari kuwa safi kwa sababu taka walizokusanya zinaonesha ni za muda mrefu.

RIPOTI MAALUM

# Mama asimulia alivyomwokoa mtoto mikononi mwa mganga

Na Neema Emmanuel, MWANZA



MAMA wa mtoto mwenye umri wa miaka miwili na miezi mitatu, anasimulia alivyonusurika mtoto wake baada ya kulishwa wali na uji pekee kwa miezi minne mfululizo bila kuchanganya lishe nyingine.

Baada ya hapo alikumbwa na tatizo kisha kupelekwa kwa mganga wa kienyeji kutibiwa hali ikawa mbaya zaidi, mwisho akaponea hospitalini.

Ni baada ya yeye kwenda mjini kutafuta maisha na kumwacha mtoto wake kwa shangazi yake, Maria Kasinje (42), wakati huo akiwa na umri wa mwaka na miezi saba.

Katika Kijiji cha Bubinza, Kata ya Lubugu, wilayani Magu, mkoani Mwanza, mwandishi wa habari hii anakutana na Sundi Charles (20), mama wa mtoto huyo wa kiume ambaye anasimulia kisa mkasa mzima.

Anasema mtoto wake aliacha kunyonya akiwa na mwaka na miezi mitatu na alipofikisha mwaka na miezi saba, alimwacha nyumbani kwa shangazi yake na kwenda Nyamagana kufanya kazi za ndani.

"Kama unavyojua wali ni chakula pendwa katika jamii yetu kwa sababu ya upatikanaji wake. Si wa mara kwa mara, hivyo mtu anapopikiwa huona ameoneshwa upendo wenye thamani kubwa.

"Nilipoondoka kijijini, shangazi alinisimulia kuwa alikuwa akimpikia mtoto wali kila siku na mara moja moja kumlisha uji wa mahindi usiokuwa na lishe ndani yake.

"Baada ya miezi miwili tangu niondoke nyumbani, nilianza kupokea simu kujulishwa mtoto kuugua mara kwa mara, mwili unachemka mara kulegea na kukataa kula. Alikuwa anampikia wali, maarufu kama bokoboko na kumpatia na chai," anasimulia.

Kutokana na hali hiyo, anasema mtoto alianza kuvimba tumbo na kuwa gumu, hivyo shangazi alimshauri arudi kijijini ili kumpeleka kwa mganga wa kienyeji kwa ajili ya matibabu. Anasema walimpeleka kwa mganga na kukaa kwa wiki akipatia huduma ya tiba bila mafanikio.

"Niliona kabisa ninaelekea kupoteza mtoto kwa sababu hali yake iliendelea kuwa mbaya, hivyo nikaamua kumpeleka hospitalini ambako walibaini tatizo ni lishe na alikutwa na minyoo na upungufu wa damu.

"Huwezi kuamini nilipomwacha mtoto alikuwa na kilo 11 lakini zilishuka hadi kilo nane. Niliamua kukaa na mwanangu na kufuata masharti niliyoelezwa hospitalini kwa kumpatia lishe bora na kamili," anasimulia.

Anasema kadri alivyokuwa akimhudumia kwa kumbadilishia lishe, mtoto alianza kurejesha katika afya yake. Alisema awali alikuwa hawezi kuongea mpaka wakadhani ni bubu lakini sasa anaongea.

### MTAALAM AFUNGUKA

Akizungumza na Nipashe kutoka Hospitali ya Ihayabuyaga, Dk. Mubarak Irunde, anasema tatizo la utapiamlo hujitokeza endapo mtoto akipatiwa chakula cha aina moja.

Anasema mtoto anapopatiwa chakula cha aina moja, huchangia udumavu na kudidimiza maendeleo yake ya ukuaji.

Dk. Irunde anasema mtoto anapofikisha miezi sita ndio kipindi cha kujaribu kumpa vyakula vingine tofauti na maziwa ya mama.

"Mfano hupewa maziwa tofauti na ya mama na uji mwepesi ambapo inapendekezwa kupewa uji wa dona ambapo unaweza kuongoza maziwa na sukari kidogo. Mtoto anatakiwa kupewa makundi yote ya chakula ili kumwezesha kupata virutubisho vyote vinavyotakiwa ili kumsaidia katika ukuaji mzuri na kumwepusha na udumavu," anasema.

Anasisitiza kwamba udumavu huchangiwa mtoto kutokuendelea na makuzi mazuri ikiwamo ya kiakili kwa sababu hutegemeana na vyakula hasa vyenye protini.

Pia anasema kuna dalili mbalimbali ambazo zinaonesha utapiamlo kwa mtoto zikiwamo kuvimba tumbo, miguu, uso kujaa, nywele kunyonyoka ama kutokuwa na afya, mwili kupauka, kupungua kwa uzito, mtoto kula sana lakini aonyeshi mabadiliko yoyote.

"Wazazi wanapaswa kuwaandalia watoto vyakula vinavyogusa makundi yote, pia ni vyema wakawa na bajeti ya kununua chakula cha mtoto na kuzingatia utaratibu wa kumpima uzito ili kujua maendeleo yake.

"Mtoto anapaswa kula mara tano hadi sita kwa siku unampa chakula kidogokidogo mara moja moja, unampa supu ya nyama, maziwa kwa wingi, dawa za minyoo na kumpima wingi wa damu, itasaidia kuimarisha afya ya mtoto," anabainisha.

### OFISA LISHE ANENA

Ofisa Lishe kutoka Tanzania Early Childhood Education and Care (TECEC), Jackson Yawi, anasema katika makuzi, mtoto anapaswa kupata vyakula ambavyo vinagusa makundi tofauti ili kumsaidia katika ukuaji wake hasa vyenye vitamini A, mfano viazi lishe.

Anasema kadri mtoto anavyozidi kukua, anapaswa kula walau milo minne kwa siku na milo mikuu ni mitatu ikijumuishwa na matunda, juisi asili na maji.

Yawi anasema utumiaji wa aina moja chakula ni tatizo kwa sababu haukidhi mahitaji ya mtoto katika lishe ambaye anapaswa kupata virutubisho vingine.

Anasema kuna madhara mbalimbali ambayo mtoto anaweza kuyapata kwak utumia aina moja ya chakula, ukiwamo utapiamulo ambao unaweza kusababishwa na lishe hafifu au lishe duni ambayo huchangia kuingia katika hali ya ukondefu na udumavu.

Pia alisema hali hiyo huchangia upungufu wa madini chuma na kupungukiwa baadhi virutubisho muhimu ambayo inachangia mtoto kuwa na uelewa mdogo hasa darasani.

"Si lazima mzazi uwe na uwezo lakini unaweza kujali afya yake kulingana na mazingira uliyomo. Mfano unaweza ukawa na unga wa mhogo na mahindi, ukapika uji wako wa mahindi tu wakati wa kupika ukatupia yai moja au ukapika bokoboko unatumia mboga za majani unampa mtoto inasaidia," anaelimisha.

Yawi anasema katika kutoa elimu lishe amekuwa akifikia zaidi ya wazazi 50 kwa wiki ili kuwapatia elimu kuhusu umuhimu wa lishe kwa mtoto. Anasema tatizo lililoko ni mwitikio wa wazazi wa kiume kutolipa kipaumbele suala la elimu kuhusu lishe.

Agosti 31, mwaka huu, Waziri wa Afya, Jenister Mhagama, alisema wizara hiyo inaendelea kukamilisha Sera ya Chakula na Lishe ili kukabiliana na utapiamlo na udumavu nchini kwa kujumuisha mapendekezo yaliyotolewa kwenye mkutano wa tathmini ya utekelezaji wa mkataba wa lishe.

Ripoti ya Lishe ya Watoto iliyotolewa Juni, mwaka huu, na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), inabainisha kuwa asilimia 22 ya watoto nchini wanakabiliwa na umaskini wa chakula kwa kiwango kikubwa na asilimia 59 katika kiwango cha kati, hali inayohatarisha ukuaji wao.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, asilimia 27 ya watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano, sawa na watoto milioni 181 wanapata milo isiyozidi miwili kati ya minane inayotambuliwa na shirika hilo.

Kati ya watoto hao, milioni 64 wanaishi kusini mwa Asia na milioni 54 kusini mwa Jangwa la Sahara, Tanzania, Uganda, Afrika Kusini, Somalia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) zikiwamo.

Nchi zingine ni Afghanistan, Bangladesh, China, Ivory Coast, Ethiopia, Ghana, India, Indonesia, Myanmar, Niger, Nigeria, Pakistan, Philippines na Yemen.

Miongoni mwa watoto hao, wanne kati ya watano hulishwa tu maziwa ya mama na au bidhaa za maziwa au chakula chenye wanga, kama vile mchele, mahindi au ngano; chini ya asilimia 10 hulishwa matunda na mboga na chini ya asilimia tano hulishwa mayai, nyama, kuku na samaki.

## HABARI KITAIFA

# Majaliwa asema SDG msingi wa matumaini

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amehutubia Mkutano wa 79 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UNGA79) na kusema Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG) ni msingi wa matumaini katika kukabiliana na changamoto za kidunia.

Hii ni mara ya pili kwa Waziri Mkuu wa Tanzania kuhutubia Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa. Mara ya kwanza ilikuwa Septemba 27, 2010 wakati Waziri Mkuu Mstaafu, Mizengo Pinda, alipolihutubia Baraza la 65 (UNGA65).

Majaliwa alisema hayo juzi wakati akihutubia kwenye mkutano huo ulioshirikisha wakuu mbalimbali wa nchi jijini New York, Marekani, anakomwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema chini ya uongozi wa Rais Samia, Tanzania imedhamiria kufanikisha malengo endelevu ya kiuchumi, ufugaji, uwekezaji katika miundombinu na mifumo ya kidijitali, uvuvi na nishati.

"Lengo letu ni kufikia uhakika wa kupunguza umasikini, kutengeneza ajira mpya na kusukuma mbele maendeleo ya uchumi shirikishi katika nyanja mbalimbali. "Kuna shuhuda nyingi za taarifa za makuzi katika sekta hizo Tanzania zinazotokana na mikakati kama ya Kesho Iliyo Bora (BBT) unaohusu kilimo kwa Tanzania Bara na uwezeshaji wanawake wanaoshiriki kilimo cha mwani Zanzibar.

Alisema Tanzania, kama yalivyo mataifa mengine, imekuwa ikipambana na changamoto kama za athari za UVIKO-19 kwenye sekta ya afya, mabadiliko ya tabianchi yanayojidhihirisha katika ongezeko la hali mbaya ya hewa kama mvua haribifu na ukame uliokithiri, pamoja na mambo mengine, vimeathiri ufikiwaji wa malengo endelevu.

Majaliwa alizungumzia pia Sera ya Tanzania ya Mambo ya Nje kuhusu utu kwamba Desemba 14, 1961 wakati akiwa Waziri Mkuu wa Tanganyika, Mwalimu Julius Nyerere alisema: "Msingi wa matendo yetu, ya ndani (ya nchi) na ya nje (nchi za nje) utakuwa ni kujaribu, kiungwana, kuheshimu utu wa mtu."

Alisema Tanzania imeendelea na msimamo huo katika mapambano dhidi ya ukoloni na ubaguzi wa rangi na kwamba kwa muktadha huo Tanzania ilikuwa ni mwenyeji wa Kamati ya Ukombozi wa Bara la Afrika (OAU) ikiwaunga mkono wapigania uhuru wa mataifa mbalimbali ya Afrika.

Alisema pamoja na kupatikana kwa uhuru, mataifa hayo bado yanakabiliwa na vikwazo vya kiuchumi na mazingira hatarishi kwa utu yanayokwamisha upatikanaji wa maendeleo halisi.

"Kwa hiyo tunatoa wito watu wajitawale wale ambao bado katika mifumo ya ukoloni, na kuondolewa kwa vikwazo vya kiuchumi vilivyowekwa kwa mataifa ya Cuba na mengineyo," alisema.

Alitumia jukwaa hilo kuliarifu baraza hilo juu ya uwepo wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa na uchaguzi mkuu ujao unaotarajiwa kufanyika nchini.

"Novemba, mwaka huu, Tanzania itafanya uchaguzi wa Serikali za Mitaa, kisha kufuatiwa na uchaguzi wa Rais na Wabunge Oktoba, 2025. Tunapojiandaa kwa matukio haya ya uchaguzi, ningependa kuliarifu baraza hili kuwa demokrasia, haki za binadamu, na utawala wa sheria vitaheshimiwa, sambamba na maono ya Rais Samia kama ilivyoelezwa katika falsafa ya 4R, ambazo ni upatanisho, ustahimilivu, mageuzi na ujenzi upya," alisema.

# Waziri aonya taasisi ukwepaji mfumo NeST ununuzi wa umma

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, ameagiza taasisi zote za umma kuzingatia matakwa ya sheria ya ununuzi wa umma na zinazokaidi zichukuliwe hatua kwa mujibu wa sheria.

Dk. Nchemba aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akipokea taarifa ya mwaka ya utendaji wa Mamlaka ya Ununuzi wa Umma (PPRA) kwa mwaka wa fedha 2023/24.

Alisema sheria imeweka kosa la jinai kwa mtu ambaye kwa makusudi ataamua kufanya ununuzi nje ya mfumo wa kieletroniki akibainika na kuthibitika, atapatiwa adhabu ikiwamo kifungo cha miaka mitatu jela.

"Nimesikia kuwa zipo baadhi ya taasisi nunuzi bado zinasitasita kutumia Mfumo wa Ununuzi wa Umma wa Kieletroniki Tanzania (NeST), ingawa zimewezeshwa kuutumia.

"Nazielekeza taasisi zote za umma kuzingatia matakwa ya sheria ya ununuzi wa umma na kutumia mfumo wa NeST ili kuongeza ufanisi na kuhakikisha tunapata thamani halisi ya fedha," alisema.

Dk. Nchemba alisema endapo watakuwa na changamoto yoyote wanapaswa kuwasiliana na PPRA ili wapate maelekezo na idhini ya hatua zinazopaswa kuchukuliwa.

"Haiwezekani taasisi imepatiwa elimu ya kutumia mfumo huo alafu hawatumii, jambo hilo halipo sawa taasisi zinazokwamisha wasione aibu kuwachukulia hatua.

"Wananchi tunawataka watumie EFD (mashine za risiti za kielektroniki) halafu taasisi za umma hazitaki kutumia zabuni hizo, taasisi ambazo zinakiuka taratibu za ununuzi wanatakiwa kutangazwa na kufahamika atakayefanya manunuzi nje ya mfumo sheria ichukue mkondo wake," alisema.




Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba (kushoto), akipokea taarifa ya Tathmini ya Utendaji Kazi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), kwa mwaka wa fedha 2023/2024, kutoka kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya PPRA, Dk. Leonada Mwagike, jijini Dar es Salaam, jana. Kulia ni Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, Dennis Simba. **PICHA: WF**

Dk. Nchemba alisema ni marufuku kuagizwa kwa thamani nje ya nchi na yoyote anayehitaji aagize kwa ajili ya nyumbani kwake na sio kwa matumizi ya serikali.

"Ni muhimu kutumia bidhaa zinazozalishwa hapa nchini mtu anaagiza mawe nje ya nchi ama nondo wakati zinazalishwa hapa nchini huko ni kuongeza gharama. Kama nondo unazozitaka hazipatikani, ingia makubaliano na kiwanda kikutengeneze ukubwa unaoutaka. Tuache mazoea ya kuagiza malighafi nje ya nchi wakati zinapatikana nchini," aliagiza.

Alisema mfumo huo umesaidia kuboresha mifumo ya udhibiti wa ndani wa taasisi nunuzi na hivyo kuendana na tamko la la Rais Samia Suluhu Hassan, kuitaka Wizara ya Fedha kudhibiti matumizi ya fedha za serikali hasa katika utekelezaji wa miradi.

Alisema bado wana kazi kubwa ya kujenga uwezo na kuhamasisha jamii kuanza na kuendelea kutumia mfumo huo.

Alisema mtokeo chanya ya mfumo huo ni pale mwananchi wa kawaida watakapoweza kupata huduma na bidhaa kwa bei nafuu kulingana na thamani ya fedha.

"Ni muhimu, Bodi ya Wakurugenzi sasa ikaweka mkakati mzuri ili kuhakikisha tunakamilisha ujenzi wa mfumo wa NeST katika moduli mbili zilizosalia kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha 2024/25," alisema.

Alisema pia, kuendelea kutoa usaidizi kwa watumiaji wa mfumo ili wizara na nchi iweze kupata faida ya matumizi ya mfumo wa kidigitali na hivyo kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi PPRA, Dk. Leonada Mwagike, alisema licha ya mafanikio ambayo wameyapata, ziko changamoto zikiwamo baadhi ya taasisi nunuzi kutotumia mfumo wa kieletroniki katika michakato ya ununuzi.

Alisema hadi kufikia Juni 30, mwaka huu, taasisi za ununuzi zilipanga kuwa na zabuni 99,671, lakini ni zabuni 53,886 ndizo zilizotangazwa kupitia mfumo wa NeST.

Alitaja changamoto nyingine ni baadhi ya taasisi nunuzi kutokutenga asilimia 30 ya bajeti yake ya ununuzi kwa ajili ya makundi maalum, yaani wanawake, wazee, vijana na watu wenye mahitaji maalum.

Mwagike alisema mamlaka itachukua hatua kwa kuzishauri hatua za kinidhamu kwa wale wanaokiuka matakwa ya sheria kwa mamlaka husika.

Alisema wameokoa jumla ya Sh. bilioni 14.94 kupitia ukaguzi na Sh. trilioni 2.7 kupitia ufuatiliaji.

# Zanzibar yaongeza bajeti elimu ya juu

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imeongeza bajeti ya elimu ili kuwawezesha vijana zaidi kunufaika na mikopo na kuendelea na elimu ya juu.

Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, aliyasema hayo jana Tunguu, wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja kwenye Mahafali ya Wanafunzi wa Vyuo na Vyuo Vikuu Zanzibar, yaliyoandaliwa na Umoja wa Vijana (UVCCM) katika ukumbi wa Dk. Ali Mohamed Shein, Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA).

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Idara ya Mawasiliano Ikulu, Zanzibar, Rais Mwinyi alisema serikali imeongeza bajeti ya elimu kutoka Sh. bilioni 265.5 kwa mwaka 2021/22 hadi Sh. bilioni 851 mwaka 2024/25, sawa na ongezeko la asilimia 221.

Dk. Mwinyi aliwahakikishia vijana wote wanaopata fursa ya kujiunga na elimu ya juu kuwa watapata mikopo isiyo na masharti na kusema serikali imeongeza bajeti ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Zanzibar kutoka Sh. bilioni 4.0 mwaka 2011 hadi Sh. bilioni 33.50 mwaka 2024.

Alibainisha kwamba kiwango hicho cha fedha kinawasomeshea vijana 7,367 wa elimu ya juu kwa kuwanufaisha wanaosoma vyuo vya ndani na nje ya Tanzania.

Dk. Mwinyi alisema ili kuhakikisha vijana wengi zaidi wananufaika na fedha hizo, tayari serikali imeanza kutoa mikopo kwa wanafunzi wanaosoma ngazi za stashahada.

Aidha, Dk. Mwinyi aliwaelezea wanafunzi 365 wenye ufaulu bora zaidi wa daraja la kwanza wananufaika na ufadhili unaotolewa na Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali nchini.

Kadhalika, alisema serikali imeimarisha mafunzo ya amali kwa kujenga miundombinu imara ya fani za ufundi wa aina tofauti inayofundishwa kwa vyuo vya mafunzo ya amali nchini ili kuwajenga kiuweledi wahitimu wa vyuo hivyo wanapomaliza masomo yao wajiajiri na kuajiriwa.

Aliwataka vijana kutumia fursa ya elimu iliyopo kwa kujiendeleza pamoja na kuongeza maarifa ya kitaalmu waliyoyapata kipindi cha mafunzo yao.

Kuhusu ujenzi wa vyo vikuu, Rais Dk. Mwinyi alisema tayari serikali imeanza ujenzi wa vyuo vyengine vipya vitano vya mafunzo ya amali Unguja na Pemba ili kutoa fursa zaidi kwa vijana wengi kupata ujuzi na maarifa ya kukabiliana na changamoto ya ukosefu wa ajira.

Alisema ujenzi wa vyuo hivyo ni jitihada za serikali anayoiongoza za kuimarisha uwekezaji kwenye huduma za jamii na ujenzi wa miundombinu ikiwamo ya barabara, viwanja vya ndege, bandari, masoko na kuhamasisha wawekezaji wa sekta ya utalii na ujenzi wa viwanda, ni miongoni mwa dhamira za kuongeza fursa za ajira na kukuza uchumi wa nchi.

Kuhusu mafanikio ya miaka minne ya uongozi wake husussan kwenye ajira, Dk. Mwinyi amebainisha miradi 330 yenye mtaji wa dola za Marekani bilioni 5.4 imesajiliwa na kutegemewa kuzalisha zaidi ya ajira 18,000 kwenye uwekezaji na shughuli za biashara.

Alisema juhudi hizo zinakwenda sambamba na uwezeshaji wa wananchi kiuchumi wakiwamo vijana kupitia "Programu ya Inuka" na serikali iliweka Sh. bilioni 15 za mikopo yenye masharti nafuu inayotolewa kwa wananchi.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Elimu zaidi kuhusu wosia inahitajika kwa wananchi

**KWA** miaka mingi nchini, migogoro kuhusu mirathi na kugombea mali katika familia mbalimbali imekuwa ikiongezeka hata kusababisha baadhi ya wahusika kuuawa au kupata ulemavu wa kudumu.

Chanzo kikubwa cha kuwapo kwa madhila hayo ni Watanzania wengi kushindwa kuandika wosia wakati wakiwa hai. Hatua hiyo husababisha kuibuka kwa migogoro ndani ya familia kutokana na kugombania mali za marehemu na wakati mwingine mama na watoto, mara baba anapoaga dunia, hufukuzwa kwenye nyumba na kuporwa mali na baba wadogo, wakubwa na mashangazi.

Kwa familia zile ambazo zimekuwa zikisimama imara na kuweka misimamo dhidi ya ndugu wa marehemu kuchukua mali hizo, zimekuwa zikifanyiwa mauaji yakiwamo ya kinyama kwa kuchomwa moto na kuteketea wakiwa ndani ya nyumba. Matukio hayo yamejitokeza kwa kiasi kikubwa katika baadhi ya makabila yanayoendekeza mfumo dume kwamba mwanamke hawezi kurithi mali za mume.

Sababu kubwa au kasumba iliyoenea miongoni mwa Watanzania kutokuandika wosia ni imani katika jamii kwamba kufanya hivyo ni uchuro. Wako baadhi ya watu ambao wanaamini kwamba kuandika wosia ni kujitabiria kifo.

Licha ya kuwapo kwa madhara hayo, baadhi ya familia zimekuwa zikipata matatizo kama vile watoto kukatisha masomo kutokana na akaunti za wazazi kusimamishwa hadi mrithi atakapopatikana. Hali hiyo husababishwa na migogoro na mashauri ya mirathi kuchukua muda mrefu kwa sababu ya kuwapo kwa mivutano katika baadhi ya familia baina ya ndugu upande mmoja na mke na watoto wa marehemu upande mwingine.

Mbali na mivutano hiyo, wako baadhi ya watu ambao wamekuwa wakichukua mali za marehemu kwa nguvu na wakati mwingine, kutokana na mashauri ya mirathi kuchukua muda mrefu, baadhi ya mali zimekuwa zikipotea au kuharibika. Jambo hilo husababisha hasara kwa baadhi ya wanafamilia kwa kuwa mali hizo zingewawezesha kuzitumia kwa makusudi mbalimbali.

Kuwapo kwa hali hiyo, kumesababisha serikali na wadau mbalimbali, wakiwamo wanaharakati wa kutetea haki za binadamu kutoa elimu kuhusu umuhimu wa watu kuandika wosia. Jitihada hizo zimekuwa sawa na kutwanga maji kwenye kinu kwa kuwa mwitikio umekuwa mdogo.

Jambo la kufurahisha ni kwamba serikali haijakata tamaa katika kuwahimiza watu kufanya hivyo. Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Jumanne Sagini, ameendeleza jitihada za serikali kutaka elimu hiyo itolewe kwa wananchi ili kujua muhimu wa kuandika wosia. Katika kufanya hivyo, ameshauri itafutwe njia ya kuwasaidia wananchi kuondoa hofu ya kutokuandika wosia ili kupunguza migogoro kipindi cha mirathi.

Akiwa katika ziara kwenye Kituo Jumuishi cha Masuala ya Familia Temeke kwa ajili ya kujifunza mambo mbalimbali na kuona shughuli za kimahakama zinazotolewa kwa wananchi jana, Sagini alisema hali hiyo inatokea kwa sababu wananchi wengi hawaelewi umuhimu wa wosia. Kutokana na hali hiyo, alisema elimu bado inatakiwa kutolewa katika jamii ili kuondoa mgongano au kutofautiana kwa wanafamilia.


Kurudiwa kwa msisitizo huo kuhusu elimu na mwitikio kuwa mdogo imekuwa sawa na maagizo muhimu kutolewa na hatimaye kufikia katika masikio ya viziwi. Kwa maneno mengine, imekuwa sawa na viongozi wa dini kuwataka waumini wao kuacha dhambi na wao kusikia na kuendelea na mambo hayo kama kawaida.

Ni dhahiri kwamba tatizo la watu kushindwa kuandika wosia limekuwa sugu kwa sasa ndiyo maana kuna migogoro mingi ndani ya familia za kitanzania. Kama ni ngoma kuhusu mirathi imepigwa kwa kiasi kikubwa, hivyo ni muhimu kwa Watanzania kutekeleza ushauri huo kwa maisha yao.

Kama wahenga wasemavyo asiyesikia la mkuu huvunjika guu, vivyo hivyo kuendelea kupuuza ushauri kuhusu kuandika wosia ni sawa na kukubali kuingia katika matatizo licha ya kuambiwa mara kwa mara. Shime Watanzania wasikie wito huo na kuufanyia kazi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# TANROADS waepusheni watu na ajali za barabarani

Na Sabato Kasika

**PEMBENI** mwa Barabara ya Morogoro eneo la Mbezi Mwisho, Dar es Salaam, kumejengwa uzio kwa lengo la kutaka kuepusha watu kugongwa na magari wanapovuka upande wa pili wa barabara hiyo.

Badala yake, watumie daraja la waenda kwa miguu lililopo eneo hilo, kwa ajili ya usalama wao. Hata hivyo, licha ya Wakala Barabara Tanzania (TANROADS), kuweka uzio huo, kuna jambo haliko sawa.

Kwa nini? Kwa sababu bado watu ambao hawataki kuvuki upande wa pili wa barabara kwa kutumia daraja, badala yake, wanapenya kwenye uzio huo bila kujali usalama wao.

Mtindo huo umesababisha wakang'oe baadhi ya vyuma vya uzio huo ili waweze kupata upenyo mkubwa zaidi wa kupita, kitendo ambacho ninakiona kama hujuma kwa TANROADS.

Ingekuwa vyema kama TANROADS watawaepusha kutoka katika mazingira hayo hatarishi kwa kuwalazimisha kupita juu ya daraja kabla hawajagongwa na magari. Lakini njia ya pili ninayoiona, ni kuwakamata kwa kuharibu huko ambako ninaamini ujenzi umetumia fedha nyingi za walipa kodi na sasa unaharibiwa na watu wachache wasiozingatia maelekezo.

Vilevile, si vibaya TANROADS ikaongeza vyuma kwenye uzio huo ili kusiwepo upenyo wa kuwawezesha kupita kama wanavyofanya sasa. Hatua hiyo iende sambamba na kuulinda usiendelee kuharibiwa.

Kwa vitendo vinavyoendelea katika eneo hilo, ni wazi wameshindwa kutii sheria bila shuruti, hivyo, si vibaya wakashurutishwa kutii sheria ili wasiendelee kuharibu miundombinu hiyo muhimu kwa usalama wao.

Inashangaza kuona watu wanaamua kufanya vitendo hivyo mchana kweupe huku kukiwa hakuna mtu anayejali, kitendo kinachofanya waone kuwa wana haki kuharibu uzio huo.

Ninadhani wanafanya hivyo, kwa sababu wanajua hakuna wa kuwafuatilia, lakini kama TANROADS wangefuatilia kimya kimya wangenesa wengi hasa wapiga debe na mama lishe.

Watu hao hawaoni shida kupenya chini ya uzio au kwenye nafasi kati ya chuma kimoja na kingine ili wavuke upande wa pili bila kuhofia kugongwa na magari, bila kujali wanaharibu miundombinu.

Yote hayo yanasababishwa na mtindo wa watu wa kutojali wala kuheshimu utaratibu, kwani imekuwa ni kawaida hata kama wamewekewa tangazo la kuwazuia, huwa hawazingatii.

Kwa mfano unaweza kukuta limewekwa tangazo kuwa ni marufuku kufanya biashara eneo fulani, lakini eneo hilo ndilo unakuta watu wamepanga biashara tena bila hofu.

Aidha, unaweza kukuta ujenzi unaendelea sehemu fulani, huku kukiwa kumewekwa utepe mwekundu, unaoshirikia kuwa haruhusiwi mtu kupita eneo hilo la kazi, lakini ajabu ni kwamba watu hulazimisha kupita.

Sasa kwa mazingira kama hayo, ni wazi kuna jambo la ziada ambalo serikali inatakiwa kuzichukua kwa wananchi wake. Kuwaelemisha kujua umuhimu wa kutii au kuwalazimisha kutii bila shuruti.

Njia hizo zikitumika, zinaweza kuwaokoa Watanzania dhidi ya ajali zinazowanyemelea kutokana na wao wenyewe kutozingatia utaratibu na kufanya mambo wanavyotaka bila kuzingatia mazingira waliomo.

Katika maeneo mbalimbali ya jiji la Dar es Salaam, ni kama haishangazi kuona wamachinga wakiwa wamepanga biashara zao hadi kuziba sehemu ya barabara bila kuhofia kugongwa na magari.

Hata kama kuna bango kubwa lenye maandishi yanayoeleza kuwa ni marufuku kufanyia biashara eneo hilo, wao hilo haliwahusu. Mtindo huo unahatarisha maisha yao kama wanavyofanya wale wasiotaka kuvuka barabara kwa kupita juu ya daraja.

Fikiria kwamba, kama gari litamshinda dereva, ni rahisi 'kuwavaa' wafanyabiashara hao na kusababisha maafa, kwani wengi wao wanafanyia biashara katika mazingira hatarishi.

**MAKALA**

**FIKRA MBADALA**

# Kama hawa wameweza, wengine tunakwama wapi?



Pascal Mayalla

MARA yangu ya kwanza kutinga New York, kutembelea Makao Makuu ya Umoja wa mataifa (UN) nilitembezwa sehemu mbalimbali huku nikitambulishwa kwa wafanyakazi wa umoja huo ambao ni Watanzania, ukiondoa UN Radio.

Huko kwingine kote, Watanzania ni wa kutafuta kwa tochi. Wenzetu Wakenya, Waganda na Wasomali wako kibao! Nikamuuliza mwenyeji wangu kwa nini Watanzania ni wachache kulinganisha na majirani zetu? Jibu alilonipa ni kwamba UN wanaajiri kwa 'quota system' na Tanzania iko kwenye kundi la Afrika mashariki na Pembe ya Afrika. Akasema Watanzania hawa wanaomba kazi UN kila zinapotokea nafasi za kazi na wachache wanaoomba hawawezi kushindana, hivyo wenzetu wanatushinda. Nikajiuliza ni hatuna uwezo au?

Nikafarijika kukutana na binti mmoja ni Mtanzania Mzanzibari ni meneja wa CitiBank New York, nikaja kukutana na binti mwingine Mtanzania, binti wa Kitanga, ni Meneja benki ya Standard Chartered London lakini sikubahatika na kukutana na Watanzania amba oni maofisa watendaji wakuu wa kampuni za Kimataifa.

Tanzania ni nchi iliyobarikiwa sana na Mungu. Ina watu wakarimu, watulivu na wasio na fujo wala vuurugu. Ina ardhi kubwa ya kutosha yenye udongo wenye rutuba kuotesha kila aina ya mazao ya chakula na biashara kuilisha Afrika na dunia lakini kitu cha ajabu ni kwamba tunaagiza vyakula kutoka nje na vingine vinatoka kwenye vinchi vidogo ambavyo havina kitu kulinganisha na sisi!

Tanzania tuna vyanzo vingi vya maji, mito, vijito, maziwa na chemchem kuweza kuendesha skimu za kilimo cha umwagiliaji. Kitu cha ajabu Tanzania, kilimo chetu ni cha kutegemea mvua badala hata kuvuna hayo maji ya mvua kwa kuchimba mabwawa, na kulima mwaka mzima.

Pia Tanzania ndiyo nchi inayoongoza duniani kwa kivutio kikubwa kabisa cha utalii. Ziko mbuga za Wanyama kama Serengeti, Mikumi, Ngorongoro, Ruah ana Udzungwa. Kwa Afrika tuna vivutio vingi na vizuri vya asili kuliko nchi zote lakini ukiangalia idadi ya watalii wanaotembelea Tanzania ulinganishe na nchi zingine ambazo hazina hata nusu ya tulicho nacho, utaishia kushangaa. Eti Tanzania ni ya tano kwenyekati ya nchi 10 zinazotembelewa na watalii wengi Afrika! Tumepitwa na Kenya!, nusu ya watalii wa Kenya wanakuja kupanda mlima Kilimanjoro! Kenya inautangaza zaidi kuliko wenye mlima wenyewe!

Tanzania tunayo madini mengi na ya thamani mfano Tanzanite, inayopatikana Tanzania pekee lakini ukiangalia urari wa mauzo kwenye soko la dunia, ni nchi ya nne kuuza Tanzanite, ya kwanza ikiwa India ikifuatiwa na Afrika Kusini na Kenya. Mtu unajiuliza kama Tanzanite inaptikana Tanzania pekee, hao India, Afrika Kusini na Kenya hizi Tanzanite wanayoiingiza kwenye soko la dunia wanaitoa wapi?

Aidha, Tanzania ni nchi ya tatu kwa utajiri wa dhahabu Afrika ikitanguliwa na Ghana na Afrika Kusini na ni nchi ya 16 duniani, Tuna migodi mingi na ukiondoa mmoja tu wa Stamigold kule Biharamulo, unaomilikiwa na Shirika la Madini Tanzania (STAMICO), mingine yote inamilikiwa na wageni na ukifika migodini, wazungu wanapishana. Menejimenti zote ni wazungu na kuna baadhi kuna Watanzania wachache wa kuzugia tu.

Sasa tumegundua gesi asili, tunauza vitalu vya gesi kwa mnada kianzio ni dola milioni moja. Mpaka sasa tuna mikataba 21 ya gesi asili na hakuna hata kampuni moja ya Kitanzania wala ya Kiafrika. Pia sijabahatika kumsikia Mtanzania yeyote yuko katika ngazi za juu za menejimenti kwenye kampuni hizo za gesi.

Hali hii ni tofauti kwa kampuni ya kwanza ni Total Energies na sasa Helios Towers, inayoongoza kwa miundombinu ya mawasiliano kwa njia ya minara ambayo imepongezwa kwa kuing'arisha Tanzania kitaifa, Afrika na kimataifa baada ya kuuvutia mkutano wa nane wa Connect 2 Connect (C2C) Afrika 2024 kufanyikia Tanzania. Helios akiwa ndiye mdhamini mkuu wa mkutano huo.

Kilichonigusa kuhusu hii Helios, japo ni kampuni ya Uingereza na iko kwenye nchi tisa zikiwamo nane barani Afrika na moja Oman, mkurugenzi mtendaji wa Helios Tanzania na mkurugenzi wa Kanda ya Mashariki ya Afrika ni Mtanzania, Gwakisa Stadi. Kati ya nchi nane za Afrika ambazo Hellios iko, mabosi wa nchi tatu ni Watanzania. Pia jambo zuri hata bosi wa kwanza kuanzisha Helios Oman ni Mtanzania.

Huu ni uthibitisho Watanzania wana uwezo wa kushika nafasi za juu za kimataifa kama watajengewa uwezo. Kama kwenye Helios Watanzania wameweza, huko kwingine tunashindwa nini au tunakwama wapi?

Kitu kizuri kuhusu menejimenti za Helios, wakati sehemu nyingi wanawake wakiwekwa nyuma na sehemu zingine ni wa kutafuta kwa tochi, menejiment ya Helios Tanzania kwenye usawa wa kijinsia ni asilimia 50 kwa 50 na wafanyakazi wa Helios Tanzania ni Watanzania kwa asilimia 100.

Kitu kingine kizuri kuhusu Helios, kila kwenye mnara wa Helios, jamii husika hufaidika kwa kupatiwa misaada ya kijamii. Mfano baada ya mkutano, menejimenti ya Helios ikiongozwa na Gwakisa Stadi, walikwenda kutoa msaada wa chumba cha kompyuta shule ya sekondari ya jamii ya Wafugaji ya Endevesi, iliyoko Oljoro na kutoa msaada wa kompyuta 28.

Kampuni ngapi za kibiashara zinafanya biashara vijijini, mfano migodini wanaishi kama peponi, vijiji jirani kwa nini wanaishi katika lindi la umasikini uliotopea, wakati hiyo dhahabu inayovunwa ni yao? Kwa waliofika Mwadui enzi za Williamson Diamond na vijiji vya jirani, waliofika Geita enzi za GGM na vijiji jirani, Gesi ya Mtwara, Bomba la Mafuta la Lindi na vitegauchumi vya uwekezaji, kwa nini wasiinge mfano wa Helios Towers?

**Wasalaam**
**Pascal Mayalla**

# Waziri apigia chapuo vijana wabunifu TEHAMA

**Na Lusungu Helela,** DODOMA

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deus Sangu ameitaka Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) kushiriki kwenye Maonesho mbalimbali ya ubunifu.

Kwa kufanya hivyo, amesema itaonesha uzuri wa mifumo iliyobuniwa na umahiri wa vijana waliondaliwa na taasisi hiyo ili vijana hao kupata soko kwenye sekta binafsi.

Sangu alisema hayo jana wakati akifunga mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi 65 wa vyuo vikuu mbalimbali yaliyofanyika kwa muda wa wiki 10 katika Kituo cha Ubunifu na Utafiti cha eGA, jijini hapa.

Alitaka eGA kutekeleza programu hiyo ya kukuza ubunifu katika teknolojia ya Habari na mawasiliano (TEHAMA) kwa wanafunzi wa elimu ya juu kimkakati kwa kuwakutanisha vijana hao na waajiri ambao ni sekta binafsi.

Pia aliitaka eGA kuimarisha ushirikiano zaidi na sekta binafsi ili vijana wanaoandaliwa na taasisi hiyo kukidhi hitaji la soko la ndani na nje ya nchi katika eneo la TEHAMA bunifu.

" Nimefarijika kusikia Benki ya NMB na kanmpuni ya Vodacom ni miongoni mwa washirika wenu ambao mnashirikiana nao kwa kuwaeleza mahitaji ya soko, hivyo kuisaidia jinsi ya kuwapika vijana ili waendane na hitaji la soko," alisema.

"Nimeambiwa mwaka jana NMB ilichukua vijana wanane mliowaandaa. Hii ni habari njema sana kwetu kama serikali," aliongeza.

Katika hatua nyingine, Sangu aliitaka eGA kuandaa kanzidata kwa vijana wote wanaopata mafunzo kwa vitendo katika Kituo hicho badala ya kuwaacha tu bila kuwa na taarifa zao.

Amesema ili kuhakikisha TEHAMA inatoa matokeo tarajiwa kwa uchumi wa Tanzania, vijana hao wanadiwe kwa ubunifu wanaofanya ili kuwashawishi waajiri.

Mkurugenzi Mkuu wa eGA, Mhandisi Benedict Ndomba, alisema kituo hicho kimekuwa kikifanya utafiti katika maeneo yote ya TEHAMA kwa kuwa utafiti huo na ubunifu unaiweka nchi katika nafasi nzuri ya kushindana kwenye uchumi wa kidijitali na mataifa mengine.

Naye Jane Claud, ambaye ni mwanafunzi aliyepata mafunzo kwa vitendo katika kituo hicho, licha ya kushukuru kwa kupata fursa hiyo aliiomba serikali kuharakisha ujenzi wa kituo kikubwa ili kuendana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia yanatokea duniani.

# Elimu ya lazima miaka 10 rasmi 2027

**Na Grace Mwakalinga**

SERIKALI imesema utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la Mwaka 2023, kuhusu elimu ya lazima kuwa ya miaka 10 kuanza mwaka 2027/28.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, aliyasema hayo juzi mkoani Ruvuma kwamba wahitimu wa elimu ya msingi ya miaka sita watakutana na wahitimu wa mwisho wa elimu ya msingi ya miaka saba na wataanza kidato cha kwanza kwa pamoja.

Akiwasilisha mada kuhusu sera hiyo kwa wajumbe wa Baraza Kuu la Umoja wa Wanawake wa Chama cha Mapinduzi, Wenyeviti na Makatibu wa Wilaya Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Prof. Mkenda alisema:

"Toleo hilo lina maelekezo kwamba ifikapo mwaka 2027/28 mtoto ambaye hatakaa shuleni kwa miaka 10, hatua za kisheria zitachukuliwa kwa mzazi au mlezi."

Prof. Mkenda alisema katika kuhakikisha utekelezaji wa Sera unafanikiwa, serikali inaendelea na kufanya mapitio ya Sheria ya Elimu, Sura ya 353, ili iendane na mabadiliko yaliyomo katika Sera mpya na mapitio hayo yatakapokamilika yatapelekwa bungeni .

"Tumeamua mtoto akae shuleni miaka 10, anaanza shule akiwa na miaka sita akifika darasa la saba anakuwa na miaka 13.

"Tunasema elimu ya lazima imekwisha, tunampa mtoto wa miaka 13 hiari ya kuamua kusoma au kutokusoma, je, amefikia umri wa kufanya uamuzi? Lakini akikaa kwa miaka 10 atatoka akiwa na miaka 16," alisema.

Alisema utekelezaji wa mitaala mipya unakwenda kwa awamu na kwamba, umeanza kutekelezwa kuanzia elimu ya awali, darasa la kwanza na wanafunzi ambao watamaliza darasa la sita mwaka 2027 watalazimika kuendelea na kidato cha kwanza mpaka nne kwa lazima na kwa upande wa sekondari walioanza na mitaala mipya ni wa mkondo wa Amali.

Katibu Mkuu Wizara hiyo, Prof. Caroylne Nombo, alisema kuwa wanafunzi wanaosoma mkondo wa Amali watalazimika kusoma masoma matano ya lazima pamoja na moja la fani atakayochagua kutoka katika fani kuu 15 za katika mkondo huo.

Prof. Nombo aliyataja masomo hayo kuwa ni pamoja na hisabati, kiingereza cha mawasiliano, elimu ya biashara ambalo ni lazima kwa wanafunzi wote historia ya Tanzania na maadili ambalo litafundishwa kwa Kiswahili na atapaswa kuchagua lugha ya pili atakayoichagua.

"Shule 28 za serikali zimeanza kutoa mafunzo ya elimu ya Amali na tunategemea kuongeza shule za Amali ili vijana waingie katika kada mbalimbali za amali watakapomaliza masomo yao waweze kujiajiri au kuajiriwa na wanaweza pia, kuendelea na Diploma na kwenda kusoma Shahada ya fani aliyochagua," alisema Prof. Nombo.

Mjumbe wa mkutano huo, Hawa Ghasia, alisema kuwa mageuzi hayo ya Sera ya Elimu inaleta matumaini makubwa kwa kuiona nchi katika miaka 10 ijayo namna vijana watakavyokuwa katika mazingira mazuri.

# Mradi 'Rudi Shule' waondoa mkwamo wa kielimu watoto

**Na Elizabeth Zaya,** TABORA

BAADHI ya wanafunzi wa Sekondari ya Isagenhe, wilayani Nzega, mkoani hapa, wameelezea namna mradi unaojulikana kama 'Rudi Shule' unaoendeshwa na Shirika la Msichana Initiative unavyowasaidia kuwaondoa katika mkwamo wa masomo yao.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti na waandishi wa habari walioko katika ziara maalumu inayojulikana kama 'Caravan' inayofanywa na Mtandao wa Kutokomeza Ndoa za Utotoni Tanzania(TECMN) katika mikoa minne, walisema mradi huo umesaidia kutoa motisha hususani kwa wanafunzi wa kike kuendelea na masomo yao.

Mwanafunzi wa Kidato cha Tatu, Jane Chembamoyo, katika shule hiyo, alisema vipo vikwazo vingi ambavyo vimekuwa vikiwakwamisha wanafunzi wengi kushindwa kuendelea na masomo yao.

Chembamoyo alivitaja kuwa ni pamoja na kukosa mahitaji ya msingi ikiwamo sare za shule, daftari na taulo za kike, lakini tangu mradi huo upelekwe shuleni kwao wengi wao wanajituma na masomo.

"wanza katika jamii yetu hii, wazazi wengi hawapendi kuwapeleka watoto wao shuleni hasa wa kike, huwa wanapenda waolewe tu ili wapate mahali, kwa hiyo unakuta wanakutengenezea visababu vya kukufanya ukate tamaa uache mwenyewe kwenda shuleni.

"Na mitego mingi ipo pale unapohitaji daftari, sare za shule na mahitaji mengine yote ya shuleni, huwa wanasingizia kwamba hawana uwezo wa kununua ili tu wakukatishe tamaa uache, wakuozeshe, na wapo wenzetu wengi wanaacha kwa sababu hizo," alisema mwanafunzi huyo,

Alisema Msichana Initiative kupitia mradi huo wa Rudi Shule, wamekuwa wakiwasaidia kuwapatia mahitaji hayo muhimu ya shule ikiwamo baiskeli kwa wanafunzi wanaotoka umbali mrefu.

"Na hii imesaidia wengi kupata hamasa ya kuendelea na masomo, hata wazazi wakileta visingizio vyao kwa sasa tunawacha," alisema.

Anastazia Adamu, anasema yeye alikuwa anakwama wakati mwingine kwenda shuleni kutokana na umbali mrefu na hivyo kutokufanya vizuri katika masomo yake, lakini baadaye alikuwa miongoni mwa wanafunzi waliosaidiwa baiskeli.

Rosemary Batoba, Ofisa Miradi kutoka Shirika la Msichana Initiative, Wilaya ya Nzega, alisema kupitia mradi huo, wamefanikiwa kuwasaidia wanafunzi 200 wilayani humo kwa kuwapatia mahitaji mbalimbali ya shuleni.

Ofisa Uchechemuzi kutoka Msichana Initiative, Jacob Maduki, alisema katika mkoa huo wana miradi sita ambayo lengo lake ni kuwasaidia wanafunzi kutimiza ndoto zao za kielimu na kuwajengea uwezo wa kujitambua na kupinga ukatili na ndoa za utotoni.

"Na kupitia programu hizi, tumepata mafanikio na mapokeo mazuri, kwa sasa jamii imeanza kutambua athari za mila potofu hasa zile za kuamini kwamba mtoto wa kike ni wa kuolewa tu.



Katibu wa Umoja wa Wazazi wa CCM wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Nachia Juma Ali (katikati), akizungumza na ujumbe wake, baada ya kufanya usafi katika Zahanati ya Kata ya Bwembwera juzi, wakiwa katika ziara ya kuhamasisha wananchi kujitokeza kujiandikisha daftari la mkazi na la mpiga kura. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Waziri ataka mbinu za kuondoa hofu Watanzania kuhusu wosia

**Na Grace Gurisha**

NAIBU Waziri wa Katiba na Sheria, Jumanne Sagini, ametaka itafutwe njia ya kuwasaidia wananchi kuondoa hofu ya kutokuandika wosia ili kupunguza migogoro kipindi cha mirathi.

Aidha, amesema hali hiyo inatokea kwa sababu wananchi wengi hawaelewi umuhimu wa wosia, kwa hiyo bado elimu inatakiwa kutolewa katika jamii ili kuondoa mgongano au kutofautiana kwa wanafamilia.

Sagini alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati alipotembelea Kituo Jumuishi cha Masuala ya Familia Temeke kwa ajili ya kujifunza mambo mbalimbali na kuona shughuli za kimahakama zinazotolewa kwa wananchi.

"Nimesikia changamoto alizozisema Mtendaji wa Mahakama Kuu Divisheni, Mary Shirima, kwamba watanzania wengi ni waoga wa kuandika wosia hasa wanaume jambo ambalo linasababisha shauri la mirathi kuchukua muda mrefu.

"Haya niwaulize humu ndani wanawake na nyie mmeshaandika wosia? kumbe hata nyie bado basi bado tunatakiwa tupate elimu ya kutosha, kwa hiyo tunatakiwa kujiuliza kwa nini wanaogopa kuandika,"alisema.

Sagini aliiomba Mahakama itafute njia ya kuwasaidia Watanzania kuondokana na hofu hiyo kwa sababu kuna haja ya wao kufanya hivyo ili kupunguza mashauri hayo kuchukua muda mrefu, wao kama wizara wapo tayari kusaidia kutoa elimu.

"Naona siku hizi katika taasisi zetu za dini kuna madarasa ya masuala ya ndoa, lakini naona kuna mapungufu kuna haja ya kukutana na hizi taasisi, kwa sababu ni sawa tukawatumia viongozi wa dini," alisema Sagini.

Baada ya kupokea taarifa hiyo, aliupongeza uongozi wa Mahakama ya Tanzania, chini ya Jaji Mkuu Prof. Ibrahim Juma kwa kusimamia mageuzi ya mahakama ikiwamo ujenzi wa miundombinu ya majengo na mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Prof. Elisante Ole Gabriel, alisema jitihada za Mahakama kuboresha huduma za utoaji haki ni endelevu na kwamba mbali na Vituo Jumuishi vya Utoaji Haki sita ambavyo vimeshajengwa, Mahakama inatekeleza mpango mkakati wa miaka mitano. Alisema mahakama za wilaya na mahakama za mwanzo 60 zinajengwa na Vituo Jumuishi vya Utoaji Haki tisa vinajengwa katika Mikoa ya Katavi, Songwe, Njombe, Songea, Lindi, Geita, Simiyu, Singida na Visiwani Pemba

Shirima alimweleza changamoto ambazo zinakabili kituo hicho katika uendeshaji wa mashauri ya familia, ikiwemo ucheleweshaji wa wananchi kuhamisha mali za marehemu kwenda kwa warithi na jamii na wadau kutokuwa na uelewa wa kutosha juu ya masuala ya mirathi na ndoa.

Naye Naibu Msajili, Frank Moshi alisema tangu kuanzishwa kwake hadi kufikia 31 Julai, mwaka huu, kituo kimeweza kuhudumia wateja 526,262, kati ya hao wanaume wakiwa 228,447, sawa na asilimia 43.4 na wanawake 297,815, sawa na asilimia 56.6 ya wateja wote waliopata huduma kwa kipindi chote.

Moshi pia alimweleza naibu hiyo kuwa kituo kimefanikiwa kusajili na kuamua mashauri ya kifamilia katika ngazi zote za Mahakama. Kwa mwaka 2021 Kituo kilisajili jumla ya mashauri 2,383 na kuamua mashauri 1,166 na kubaki mashauri 1,217.

# Othman ataja ufunguo maendeleo Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Taifa wa Chama cha ACT Wazalendo Taifa, Othman Masoud Othman, amesema chama chake kinaamini iwapo kutakuwa na mipango sahihi ya kuwawezesha wananchi kiuchumi, Zanzibar inaweza kupiga hatua kubwa kimaendeleo.

Amesema mipango hiyo ni pamoja na kuwawezesha vijana kiuchumi na hatimaye kuwa na ujira wenye heshima.

Othman ambaye pia ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, aliyasema hayo jana Micheweni, kisiwani Pemba alipozungumza wakati wa ufunguzi wa kongamano la Vijana wa Mkoa huo lenye maudhui ya mwaka mmoja wa kuelekea uchaguzi nini Jukumu la Vijana wa Zanzibar.

Aliwataka vijana wa Zanzibar kukiunga mkono chama hicho ili kwenda na sera bora za uwezeshaji zitakazowawezesha vijana kuwa na uhakika wa ajira kupitia mifumo sahihi mbalimbali kama zilivyofanya nchi zingine duniani na kufanikiwa.

Sambamba na hilo, aliwataka vijana wa Zanzibar kutoyumbishwa na siasa za kubaguana na badala yake wahakikishe wanakwenda kwa hoja badala ya shangwe ambazo hazisaidii katika kuleta ufanisi kwenye maendeleo ya kiuchumi na siasa.

Othman aliwaeleza vijana hao kwamba Micheweni kwa Zanzibar ni miongoni mwa wilaya tajiri kwa rasilimali ikiwamo bahari yenye mazao mengi ya baharini ikiwamo samaki na kilimo kuliko sehemu nyingine yoyote ya Zanzibar, hivyo kinachohitajika ni kuwawezesha wananchi kuusarifu uchumi huo na kuleta tija kwa taifa zaidi.

Alisema kutokana na chakula kinachozalishwa kwa wingi ndani ya wilaya hiyo, imekuwa ikilisha sehemu kubwa ya Zanzibar pamoja na nazi, samaki, pweza na mengineyo lakini jambo muhimu linalohitajika ni kuwepo umoja na mshikamano wa kuhakikisha chama kinawezeshwa na wananchi kuijenga Zanzibar moja itakayokuwa na uwezo wa kujenga uchumi imara.

Kwa mujibu wa Othman, hakuna taifa lolote duniani lisilokopa fedha kusaidia bajeti yake lakini pia hakuna nchi yoyote inayoweza kupiga hatua kimaendeleo kwa kutegemea mikopo mikubwa isiyo na uwiano wa kikodi na kimapato na uwezo wa kulipa deni kwa urari wenye uwiano na makusanyo ya ndani sambamba na matumizi ya kibajeti yake.

Alisema Zanzibar ina uwezo mkubwa wa kupiga hatua kiuchumi na kimaendeleo lakini kinachohitajika ni kuwapo misingi ya uongozi bora inayofuata sheria na katiba ya nchi sambamba na ushirikishwaji wa watu wote.

# MAISHA

SEPTEMBA 29, 2024

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili




Ukurasa 15


KABATI LA VYOMBO




# REMBA MACHO YAKO HIVI

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA





| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| C | ■ | S | H | I | M | O |
| H | ■ | ■ | ■ | T | ■ | N |
| I | ■ | J | I | I | ■ | G |
| M | E | I | ■ | K | O | O |
| B | ■ | M | I | A | ■ | Z |
| W | ■ | B | ■ | ■ | ■ | W |
| A | P | O | N | E | ■ | A |


## FUMBO TOTO




Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

LAO, CHA, KOO, NOA, PENDO, AGANA, PANGA, NYOKA, CHOCHEA, ONDOSHA

## TOA TOFAUTI 5




## PAKA RANGI




## AMSHA AKILI

CHORA KWA KUUNGANISHA NAMBA KUANZIA 1-29 ILI KUPATA MCHORO KAMILI




TOFAUTI ya wazazi wa hapa nchini mtoto wa Tanzania na sehemu zingine wakati anapolala inakuwa kama hivi.

Marekani mtoto anapokwenda kulala huagwa na wazazi wake "usiku mwema mwanangu"

Uingereza wazazi wanamuaga mtoto wao "Pata njozi njema mwanetu"

Hispania anapokwenda kulala wazazi humuambia "usiku mwema mpendwa wetu"

Tanzania mtoto anapotaka kulala wazazi utawasikia "Kesho uamke mapema, hatutaki kusikia umechelewa na hela ya mihogo utaikuta mezani"

**SWALI**

Makaa ya mawe yanapatikana wapi hapa Tanzania?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Anakaribia umri wa baba yangu atanioaje?

KARIBU tena msomaji tuendelee kuangaza anga za mabinti zetu. Wiki mbili mfululizo tulimjadili mama katika malezi ya familia. Nikasema jukumu la kulea na kuongoza ni la mwanamke. Mama anapaswa kujifunza jinsi ya kufuatilia watoto wake.

Awe kwenye nafasi ya kuwa rafiki na wanawe. Mzazi hapaswi kukaa pembeni katika maisha ya mtoto wake. Nafasi ya kwanza ni mzazi kama mzazi lakini nafasi ya pili ni rafiki. Chunguza tabia, usitetee tabia ya uovu ya mtoto wako.

Rafiki hujua siri nyingi za rafiki yake. Mzazi anaweza asijue mwanaye anapitia nini. Lakini rafiki atajua mtoto wa fulani anapitia nini. Ndio maana inasisitizwa hapa kwamba kuwa rafiki na mtoto wako.

Usipokuwa karibu na mwanao, yapo matatizo yatakuletea majuto, kisa ulimwacha akajisimamia mwenyewe. Hebu kisa cha binti huyu mzazi ajifunze hapo jambo!

Binti mmoja akanitumia ujumbe akitaka ushauri kutokana na wasiwasi alio nao. Akasema hivi, anti, mimi ni binti nina umri wa miaka 22. Yuko kijana nimekuwa na mahusiano naye kwa mwaka mmoja sasa.

Na tulikutana kimwili mara tatu kisha nikaamua kuacha kwa kuhisi ndani yangu namkosea Mungu. Ni kijana ambaye amenitoa ujana wangu. Tatizo ni kwamba hataki kuvumilia hadi tutakapooana rasmi.

Pia shida nyingine ni kwamba akinidanganya umri wake kuwa ni miaka 27 kumbe ni 37. Na ukweli huo niligundua kwenye kitambulisho chake cha Mpiga kura. Na umri unakaribia umri wa baba yangu ambaye ana umri miaka 43.

Msomaji wangu, binti huyu niliimuuliza maswali kadhaa ikiwa ni pamoja na elimu yake na ikiwa anapenda kuolewa na kijana huyo. Majibu yakawa ana elimu ya chuo na kwamba anaogopa kumtambulisha kwa wazazi wake kwa maana ni mkubwa sana kwake kiumri na pia anakaribia umri wa baba yake mzazi.

Binti anaendelea kusema: "Pia anataka tuendelee na mahusiano, ananiambia tutatumia njia ya uzazi wa mpango. Ananisumbua sana turudiane kwa kuwa nilitoa mimba ya mwezi mmoja.

"Naogopa kwa sasa kuwa na mwanaume kwani kila anayenitaka anataka mapenzi kwanza ndipo anioe, ingawa mimi sitaki kufanya hivyo hadi nitakapoolewa."

Swali kwamba je, huyo kijana yuko tayari kukuoa? Akajibu ndiyo. Yuko tayari kunioa na anajenga nyumba ili tuje kuishi pamoja.

Msomaji wangu, alifikia hapo nikamshauri asiruhusu tena tendo la ndoa kwani tayari alishampa mimba na wakaitoa, wakaua yule mtoto mtarajiwa. Nikamwambia uwezekano wa kumchoka haraka ni mkubwa kama hatamtambulisha mapema.

Baada ya ushauri huo, binti huyu hakuendelea tena kuchat, naamini ushauri ulimkolea.

Simulizi hii ya binti imesheheni mambo mengi na changamoto kwa wazazi ambayo hawayajui juu ya watoto wao, hasa mabinti. Kwa mfano, tupia macho maeneo haya yalijitokeza ndani yake. Umri, elimu, mahusiano ya kimapenzi, kutoa mimba na mipango ya ndoa.

Binti huyu katumbukizwa kwenye shimo lenye mambo yote hayo niliyoyaona kwa haraka haraka. Ameanzisha mahusiano na kijana aliyemzidi umri kwa miaka 15 na kijana akimzidi umri baba wa binti kwa miaka sita.

Pengine wazazi wa binti walikuwa na mipango ya kumwendeleza kielimu lakini kumbe kwa siri alishaanzisha mahusiano, alishatolewa ujana wake pasipo wazazi kujua. Kijana alishajenga nyumba ili kuwa kivutio kwa binti kuolewa naye.

> **Binti anaendelea kusema: "Pia anataka tuendelee na mahusiano, ananiambia tutatumia njia ya uzazi wa mpango. Ananisumbua sana turudiane kwa kuwa nilitoa mimba ya mwezi mmoja.**

Kwa kifupi, yote hayo wazazi hawajui. Hizi ni miongoni mwa changamoto kubwa ambazo wazazi wanapaswa kuzipatia majawabu. Binti huyu ameweza kuvuka vihunzi vyote hivyo kwa sababu wazazi wake wamekaa na kujisahau, hawako karibu kumfuatilia kujua anapitia majaribu gani.

Ninaye binti ambaye tangu akiwa mdogo nilikuwa karibu sana naye. Elimu ya msingi, sekondari hadi chuo kikuu nilikuwa namfuatilia. Macho na masikio yangu yalikuwa wazi kujua yuko wapi, anafanya nini.

Akichelewa nyumbani lazima nidadisi alikuwa wapi na akina nani ili nijue cha kufanya kumsaidia. Ni ngumu sana kumfuatilia mtoto aliyefikia balehe au kuvunja ungo, lakini mzazi anapaswa kujitoa mhanga kumuokoa kwenye uharibifu.

Wazazi jiulize, usalama wa binti zetu ukoje? Unawafuatilia au ndio basi? Je, una ushauri gani kwa binti huyo na kwa vijana wengine wenye mtizamo wa kimaisha kama huyo hapo juu? **Tuma ujumbe mfupi 0715268581. Namba pia iko WhatsApp.**

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi



# BoT iwapoke leseni wakopeshaji mtandaoni

WAKOPESHAJI fedha kupitia App za mtandaoni, ni shida kubwa katika muktadha wa kiuchumi. Wanatuhumiwa kila kona ya nchi kwa vitendo vya udhalilishaji mtandaoni.

Wanachokifanya ni haramu, najisi kwa wakopaji wenye tabia ya ama ya kutolipa au kuchelewesha marejesho.

Mdaiwa hauawi kwa matusi wala kumdhalilisha kwa ujumbe mfupi wa madeni kutumwa kwa kila mtu aliyesajiliwa kwenye simu yake. Ingawa dawa ya deni ni kulipa, si kwa kinachofanyika sasa.

Angalau serikali imetoa wito kwa watoa huduma za kifedha nchini, kufuata sheria na taratibu za huduma za fedha, ikiwemo kupata leseni ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ili kuhakikisha huduma hizo zinatolewa kwa ufanisi bila kuwaumiza na kuwadhalilisha wanufaika na hatimaye kukuza uchumi wa nchi.

BoT chini ya Wizara ya Fedha na kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, imetengeneza mikakati kupitia Sheria ya Huduma Ndogo ya Fedha ya Mwaka 2018, ili kukomesha udhalilishaji unaofanywa na baadhi ya watoa huduma ndogo za fedha kupitia mitandao ya simu.

Benki hiyo kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha imeona umuhimu wa kutoa elimu ya fedha nchi nzima ili kuwapa uelewa wananchi kuhusu namna bora ya kukopa fedha na kuweza kurejesha mkopo bila kudhalilishwa.

Mikopo inayotolewa kwa njia ya mitandao ya simu, imekuwa changamoto kubwa hasa katika ukusanyaji wa madeni kutoka kwa wakopaji, jambo linasababisha watoa huduma hao kuvunja sheria ya usiri.

Sheria hiyo inatakiwa kuwabana pamoja na mambo mengine, watoa huduma ya fedha, wanaowadhalilisha wakopaji kwa kutuma ujumbe mfupi kwa ndugu na jamaa waliochukua mikopo hiyo.

Wizara ya Fedha kupitia BoT inapaswa kushirikisha Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kampuni za simu na Jeshi la Polisi ili kuona namna bora ya kulitatua suala hili la udhalilishaji linalofanywa na watoa huduma za fedha kupitia mitandao ya simu.

Ni wajibu wa kisheria wa Idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha katika Wizara ya Fedha, kutoa elimu kwa wananchi wanaoomba mikopo ili kuwawezesha kutumia mikopo hiyo kuzalisha faida na kuweza kurejesha kwa wakati.

Mbona tunao maofisa wa Ulinzi wa Taarifa Binafsi (DPOS) kutoka Umoja wa Benki Tanzania (TBA) na Umoja wa Watoa Huduma za Mawasiliano Tanzania (TAMNOA). Wanafanya nini kuzuia haya? hebu wafanye kazi yao kwa umakini na ufanisi zaidi, ili kuhakikisha faragha na taarifa binafsi za wateja zinalindwa.

Katika dunia ya sasa ambayo matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) yameendelea kukua kwa kasi, taarifa binafsi zimekuwa bidhaa muhimu na nyeti na hii ni kutokana na matumizi yake katika nyanja mbalimbali, ikiwemo biashara, afya, elimu, na shughuli mbalimbali za serikali.

Ni lazima mkopaji apewe elimu ya kutosha, ili apate uelewa kuhusu masharti yaliyoanishwa kwenye mkataba, kwa kupewa nafasi ya kusoma na kuuelewa mkataba wa mkopo, kabla ya kuchukua mkopo husika.

Kana kwamba haitoshi, serikali iwatumie pia maofisa maendeleo ya jamii kuzungumza na wananchi kuhusu uzuri na ubaya wa App za Mtandaoni zinazokopesha fedha.

Kufanya hivyo bila shaka, kutaikomboa jamii dhidi ya watoa huduma wasiokuwa waaminifu na kuchangia maendeleo ya nchi.

Tayari BoT imetoa mwongozo kwa wakopeshaji wa kidijitali, unaowazuia watoa huduma hao kudhalilisha, kuweka mtandaoni taarifa za waliokopeshwa au kutuma jumbe kwenye kwenye namba zilizoko katika simu ya aliyekopeshwa.

Mwongozo huo uliotiwa saini Agosti, mwaka huu, unakuja katika kipindi ambacho kumekuwa na ongezeko la taasisi mbalimbali za ukopeshaji fedha mtandaoni.

Tuhuma ni nyingi lakini la kutia moyo ni BoT kupiga marufuku wakopeshaji kutumia vitisho, vurugu au njia nyingine za kumuumiza aliyekopeshwa.

Kwamba wanatumia lugha za matusi kwa mteja au wadhamini wa mteja, au namba nyingine kwenye simu yake kwa nia ya kumdhalilisha.

Iko haja sasa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, nayo kushughulika kisheria na wanaoendesha App za Mtandaoni wakitoa huduma za kukopesha fedha, kwa sababu kinachoendelea ni hatari kwa usalama wa taifa.

Mbona iko wazi tu, kwamba ni kosa kisheria kuchukua mawasiliano ya watu wengine na kuwatumia ujumbe mfupi wa maandishi inapotokea mtejan wao ameshindwa kulipa katika muda; au asipolipa na kutuma taarifa binafsi za mteja katika mitandao kwa lengo la kumdhalilisha.

Kwa ufupi, ni mambo ya ovyo sana, watu wanaweza kuchukua taarifa zako na kuzisambaza mtandaoni.

***•Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com***

HARUSI

# Usiku wa Janeth









Ilikuwa ni shangwe na vigelegele, katika sherehe ya kuagwa Janeth Richard, Ofisa mikopo wa Platinumcredit, iliyofanyika kwenye ukumbi wa Tanzanite Kimara, jijini Dar es Salaam, Agosti 27, 2020. Mwenza wake ni Bariki Mtui, Mhandisi (TAA)

# MITINDO

Na Moshi Lusonzo





## MWENDO WA KAPELO

KUNA aina nyingi ya mitindo ya mavazi ambayo yanatoa thamani na mwonekano tofauti.

Moja ya vazi linalopendwa na wanaume wengi ni kofia. Mara nyingi utakutana nao wakiwa wamevaa kofia za aina mbalimbali kichwani wakiwa kwenye harakati zao.

Kwa ujumla uvaaji wa kofia unambadilisha mtu taswira ya uso wake kwa haraka pamoja na kumjengea mwonekano unaovutia.

Wataalamu wa masuala ya urembo wanasema uvaaji wa kofia, licha ya kupendezesha sura,pia inalinda nywele kuathirika na miale ya jua.

Kofia aina ya kapelo ina muonekano mzuri kwa mbele kutokana na kuchomoza upanga unaoziba uso zinapendwa kuvaliwa na vijana.

Kwa kawaida kofia aina ya kapelo haichagui aina ya nguo, lakini ni vizuri ikatumika na nguo zinazoendana pamoja na wakati.

Kofia ya aina hii hairuhusiwi kuvaa sehemu za kazi au ofisi za kiserikali na kama zikitumika inakuwa katika shughuli maalum za kitaifa, kisiasa, kitamaduni na kijamii.

Hata hivyo kundi la vijana hasa wasanii wamekuwa wakivaa na kuzidisha mvuto wa vazi hilo kwa watu wengine.

**UNAPONUNUA**

Wakati unapofikiria kununua kofia ya Kapelo, hakikisha unakuwa makini kwa kuangalia ubora wake na rangi unayopenda.

Hakikisha ukubwa wa kofia unalingana na kichwa chako, usinunue kubwa kwani haitakuletea matokeo mazuri.

Jambo muhimu hakikisha kofia isikubane au kupwaya ili kuepuka usumbufu pale unapovaa.

UREMBO
Na Mary Geofrey



# Remba macho yako hivi

UREMBO wa macho upo wa aina mbalimbali kulingana na ladha ya mtu anayoipenda.

Leo nitazungumzia urembaji wa macho unaofahamika kama "smoky eyes" ambao hutumia vipodozi mbalimbali kama wanja, mascara na rangi ya ngozi ya macho nyeusi, hudhurungi au za mng'aro.

Jinsi ya kuremba

Hakikisha uso na ngozi inayozunguka jicho ni safi kabla ya kuanza urembo wowote usishawishike kupaka vipodozi juu ya ngozi chafu haitakaa vizuri make-up yako.

Safisha kwa kutumia brashi laini iliyochovywa kwenye maji ya moto, tumia kitambaa cheupe na usitumie sabuni au maji ya moto.

Ngozi ya uso iko rahisi kudhurika ikipata msukosuko kidogo. Sabuni huwa na kemikali nyingi na maji ya moto yanapausha uso na kama utalazimika kutumia sabuni osha uso kwa maji ya baridi kwa muda kiasi ili kuondoa kemikali zitakazokuwa zimeachwa.

Tayarisha kope zako kwa kupaka wanja mweusi kwa uangalifu au 'eyeliner' nyeusi kama ni mtu anayejiamini unaweza tumia rangi yoyote ile sababu si wote wanaweza kupaka rangi ya njano au kijani na wakajiamini na mwonekano wao.

Kwa matokeo mazuri paka 'eye shadow' za aina mbili moja ya rangi iliyokolea na nyingine iliyong'aa.

Anza na rangi iliyo light paka kwa uangalifu kuelekea kona ya nyusi kama picha chini.

Endelea kama unapenda ming'ao machoni (hususani kwa sherehe) unaweza kupaka juu ya kope zako ila hakikisha hufiki mbali na nyusi.

Kisha malizia na 'darker colour' kama picha ya kulia inavyoonyesha anzia kona ya kushoto ya jicho kwenda kulia kwa kiasi upendacho.

Linganisha macho yako yote kama yana muonekano sawa kisha unaweza kuongezea mascara kwa juu ya nyusi ikiwa ni mpenzi.

MAPISHI
Na Mary Geofrey

# Namna ya kupika biskuti

BISKUTI si lazima ununue dukani, unaweza kutengeneza mwenyewe nyumbani kwa urahisi sana tena bila gharama kubwa.

Leo tunaelekezana namna ya kupika biskuti za jam kwa urahisi na muda mfupi sana.

**Mahitaji**

Unga glasi mbili na nusu, sukari robo tatu za glasi, glasi moja ya samli, mayai mawili, baking powder vijiko viwili vya chai, Vanilla kijiko kimoja na nusu cha chai na ganda la chungwa moja.

**Mapishi**

Chukua blender na anza kuweka mayai, sukari, vanilla, samli na maganda ya chungwa, saga vizuri.

Tia unga kwenye bakuli pamoja na baking powder, mimina vitu ulivyosaga kwenye bakuli, changanya.

Punguza unga uliochanganya kidogo weka pembeni.

Unga uliobakia tia kwenya tray ya kuchomea, utandaze vizuri, tia jam juu yake.

Chukua la kukwaruzia carrot (grater) ukwaruze unga uliuopunguza juu ya jam.

Choma kwa muda dakika 20 moto wenye nyuzi 180 .

Acha ipoe kidogo, zikate vipande vya mraba sawa na hapo tayari kwa kuliwa.



MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya

# Namna ya kupangilia kabati la vyombo kwa urembo wa nyumba

KABATI la vyombo ni moja miongoni mwa samani zenye uhitaji mkubwa kwenye nyumba.

Watu waliobarikiwa kujenga au kuishi kwenye nyumba zenye nafasi za kutosha, kabati huwa ni moja ya vitu muhimu kwao kwa ajili ya kuhifadhia vyombo.

Lakini leo nataka tuzungumzie kazi nyingine ya kabati kwenye eneo la urembo kwenye nyumba.

Kama ilivyo urembo mwingine kwenye nyumba, kabati la vyombo nalo lina nafasi ya kutumikia kama urembo.

Kutumika kwa kabati kama urembo si kwa kuweka maua au urembo mwingineo ndani yake, ni kwa kutumia vyombo hivyo hivyo ambavyo badala ya kutumika kwa ajili ya matumizi ya chakula, pia vitumike kama urembo.

Ili vitumike kama urembo, kitu cha kwanza lazima kwanza tujue eneo linapopaswa kuwekwa ndani ya nyumba husika.

Jambo lingine lazima kuhakikisha kwamba vyombo vinavyowekwa kabatini ni vile vyenye mvuto au vizuri, usichukuea tu vyombo ilimradi na kwenda kuviweka humo.

Hakikisha unazingatia rangi za vyombo vyako vinavyowekwa kabatini, zisiwe zile za kuumiza macho sana na ikiwezekana rangi zake zisipishane sana na zile za vitu vyote vilivyopo kwenye nyumba yako.

Kuwa mbunifu kuvipangilia kwenye kabati ili vilete mvuto, zingatia aina na muundo wa vyombo.

Kama ni sahani, hakikisha unapangilia kuanzia zile kubwa kuelekea ndogo zake, fanya hivyo na kwa glasi, vikombe, bakuli na vinginevyo ambavyo ni vizuri unavyokuwa umeviandaa kwa ajili hiyo.

Kumbuka si lazima viwe vinatumika, vinaweza kuwa maalum kwa urembo tu na vile vya kutumia ukaviweka sehemu nyingine au katika kabati la juu la jikoni.

Na kama uwezo hautoruhusu, unaweza pia ukavitumia, lakini unapomaliza unahakikisha kwamba unavisafisha vizuri na kuvirudisha katika sehemu yake vinapopangiliwa na katika hili ubunifu zaidi unahitajika.

Katika mpangilio unaweza kuamua grasi zikae sehemu yake, au ukaamua kila shefu zikae tatu au nne kwa mpangilio mzuri, au kila aina ya chombo ulichonacho ukakitumia kwa mpangilio maalum katika shefu zote ili 'kunogesha zaidi'.





## Matumizi mengine ya makasha

Na Restuta James

WATU wengi wanatumia kasha au kontena, linalotumika kusafirisha bidhaa melini kuhifadhia mizigo ya kibiashara hasa saruji kwa wanaofanya biashara hiyo.

Wengine ambao ni wengi wanaoamua kubadilisha kabisa matumizi ya kontena, huyatengeneza kuwa ofisi na ni wachache ambao huyarekebisha kuwa nyumba au makazi ya kudumu.

Ukurasa huu unakuletea namna ambavyo kontena linaweza kubadilishwa na kuwa makazi ya kudumu au ya muda mijini na vijijini.

Wataalamu wa mapambo ya ndani wanaeleza kuwa kontena likirekebishwa vizuri linafaa kuwa makazi na hasa kwa ajili ya mapumziko (vacation).


Hata hivyo, wanaeleza kuwa 'finishing' ndiyo itakayofanya kontena liwe na mwonekano mzuri wa makazi.

Suzan Paul, anasema mwonekano mzuri wa kontena utabebwa na vioo, uezekaji, rangi, varanda itakayowekwa na mpangilio wa bustani hasa nyasi.


"Kingine muhimu ni samani na kiyoyozi kwa mikoa yenye joto. Ukiangalia mtandaoni utaona jinsi ambavyo wenzetu kwenye nchi nyingine wanavyoyabadilisha na kuwa na mwonekano unaovutia," anasema Suzan.

Anasema jambo la msingi la kuzingatia ni uezekaji mzuri kwani kontena likinyeshewa na mvua kwa muda mrefu linaweza kutoboka na kuanza kuvuja.

"Mbali ya kutumia kama nyumba na ofisi, unaweza kulifanya kontena kuwa eneo la kuogelea yaani 'swimming pool.' Kwa wenye maeneo makubwa, unaweza kujenga nyumba kubwa nzuri ya kuishi halafu ukatumia kontena kuengeneza jiko la nje au nyumba ndogo ya vijana au sehemu yako ya mapumziko," anasema.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASI
BY ABDUL KINGO - 2024
SMS - 0713 447766
HUKU NILIPO MVUA MFULULIZO WIKI SASA HAIPUMZIKI 'BANDIKA BANDUA' HATUTOKI NJE!
MSHUA KWA UONGO HUO ULIYOUTUKUZA "PITA HUKU"
'MBONA NA DENI HAVIHUSIANI?'
RAHA YA POMBE NI UGOMVI NA NGUMI ZISIZOKUWA NA REFA KILA SIKU NIKIUTWIKA LAZIMA 'NIZITWANGE' ILA WEWE MWOGA
ACHA NIWE MWOGA LAKINI SIKO TAYARI DOMO LANGU KUWA JUMBA LA MAKUMBUSHO KAMA WEWE USIYE NA MENO
JUKWAANI
'BEBI' BADO UNAHITAJI TWENDE TUKANUNUE MWAVULI WAKO UJIFUNIKE MVUA NA JUA?
NTACHEKWA KWA MATUMIZI MABAYA YA FWEDHA!
WEWE NI BWEGE SANA ULICHOKIFANYA SIO KABISA!
HUYU JAMAA HAZIMTOSHI HUWEZI KUJI-SIFU UJINGA KAMA HUU!
KWANI NIMEKOSEA KUSEMA NIMETOA TALAKA?
TALAKA NA MVUA? WE' SI CHIZI!!!
KILA MTU NA AKILI YAKE
SIO KILA AKILI INA AKILI KAMA MNAVYODHANI
SHIDA ZENU SIO ZETU KABISA TENA MTUACHE HATUTAKI SHOBO
MWENYE SHIDA NI YUPI KATI YA ANAYEKESHA WIMA KIPINDI CHA MVUA, AU ANAYE-CHAPA USINGIZI MNONO?
WAPE WAPE KWANZA WAO WAMEPANGA SISI TUMEJENGA
WAACHE SAFARI HII HATUWACHOMOI KWENYE TOPE
MIJANAMKE GANI KAMA 'MIGOBOLE' YA KIENYEJI KILA UKIINYWESHA HAIRIPUKI!
BAR
NAKUTHIKILIDHA KWA THABABU WEWE NI NKE WA NTU MMEO NKALI THANA NATHIKIA
HIVI WE' ZIMO KWELI AU MISHALE IMEPANDANA?

# Somalia yaishutumu Ethiopia

**MOGADISHU,** SOMALIA

WAZIRI Mkuu wa Somalia, Hamza Abdi Barre ameishutumu Ethiopia kwa ukiukaji wa dhahiri wa uadilifu wa eneo lake, huku mvutano kati ya majirani hao wawili ukifikia kiwango kipya katika wiki za hivi karibuni.

Akizungumza mbele ya hadhara kuu ya Umoja wa Mataifa (UN), kiongozi huyo alisema Somalia inakabiliwa na tishio kubwa kutokana na hatua za hivi majuzi za Ethiopia ambazo zinakiuka waziwazi uadilifu wa eneo lao.

"Somalia inakabiliwa na tishio kubwa kutokana na hatua za hivi majuzi za Ethiopia ambazo zinakiuka waziwazi uadilifu wa eneo letu," alisema Barre, dhidi ya hali ya nyuma ya maelewano kati ya Addis Ababa na eneo linalojitenga la Somalia la Somaliland.

Ilielezwa uhusiano wa kihistoria kati ya majirani hao wawili katika pembe ya Afrika umezorota tangu kutangazwa Januari mosi.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa hiyo inatoa ukodishaji wa miaka 50 kwa Ethiopia, nchi kubwa isiyo na bahari, wa kilomita 20 ya mwambao wa Somaliland, ambayo ilitangaza uhuru wake mwaka wa 1991.

Mamlaka ya Somaliland walibainisha kwamba baada ya kufanya hivo, Ethiopia itakuwa nchi ya kwanza kutambua rasmi jamhuri yao.

"Jaribio la Ethiopia kunyakua sehemu ya Somalia kwa kisingizio cha kupata ufikiaji wa bahari ni kinyume cha sheria na sio lazima," alisisitiza Waziri Mkuu wa Somalia kwa UN.

Kwa kujibu wa kiongozi huyo, tangu mwezi Januari, Mogadishu iliimarisha uhusiano wake na Cairo, mpinzani wa Ethiopia.

Misri ilijitolea kwa mara ya kwanza kuchangia kikosi cha Umoja wa Afrika kilichotumwa tangu mwaka 2007 nchini Somalia kupambana na wanamgambo wa Kiislamu wenye itikadi kali wa Al Shabab.

Misheni mpya (AUSSOM), inayojadiliwa kwa sasa, itachukuwa nafasi ya Atmis mnamo mwezi Januari mwakani.

**RFI**

# Rwanda yakumbwa na virusi vya marburg

**KIGALI,** RWANDA

WIZARA ya Afya ya Rwanda imethibitisha kesi za kwanza za ugonjwa wa Marburg, ikisema ni homa ya virusi vya kuvuja damu ambayo inaweza kusababisha vifo, miongoni mwa baadhi ya wagonjwa.

Kwa mujibu wa taarifa ya wizara hiyo iliyotolewa jana, Rwanda inachunguza ili kubaini asili ya maambukizi, na kwamba walioambukizwa wametengwa kwa ajili ya matibabu, licha ya kutotaja idadi halisi ya virusi hivyo.

Ilielezwa kuwa ugonjwa huo ukiwa na takribani asilimia 88 ya vifo, inahusika na Ebola na inaambukizwa kwa watu kutoka kwa popo wa matunda. Kisha huenea kwa kugusana na maji maji ya mwili ya watu walioambukizwa.

Hata hivyo, taarifa hiyo ilisema dalili za ugonjwa huo ni pamoja na homa kali, kutapika kuumwa sana kwa kichwa, maumivu ya misuli na tumbo.

Nchi jirani ya Tanzania ilikuwa na kesi za Marburg huku 2023, wakati Uganda ikikuwa na kesi kama hizo 2017.

**TRT**



Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani Antony Blinken akiwa na mwenzake wa China Wang Schiefelbein. **PICHA:MTANDAO.**

# Pakistan yakemea vita vya Israel Gaza

**ISLAMABAD,** PAKISTAN

WAZIRI Mkuu wa Pakistan Shehbaz Sharif, amesema kuwa moyo wake unavuja damu huku akikosoa kwa uchungu vitendo vya Israel kuushambulia Ukanda wa Gaza.

Kiongozi huyo alihoji jana kuwa wanadamu watawezaje kukaa kimya huku watoto wakiwa wamelala chini ya vifusi vya nyumba zao zilizobomoka.

"Nawezaje kuwafumbia macho akina mama wanaobeba miili isiyo na uhai ya watoto wao? Huu sio mzozo tu. Haya ni mauaji ya kimfumo ya watu wa Palestina wasio na hatia," alisema.

Ilielezwa kuwa hayo yalikuja baada ya Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu kusema mbele ya hadhara hiyo kuwa nchi yake inataka amani lakini yuko tayari kupambana kwa ajili ya watu wake.

Mshauri Mkuu wa Serikali ya Bangladesh, Muhammad Yunus, ambaye ameuambia mkutano huo kwamba nchi yake imepitia mabadiliko makubwa kwa kuwa nguvu ya watu wa kawaida hasa vijana imetoa fursa ya kurekebisha mifumo na taasisi nyingi za nchi hiyo.

Yunus alisema maandamano makubwa yaliyoshuhudiwa msimu huu wa kiangazi na yaliyoongozwa na wanafunzi na vijana yalilenga kutokomeza ubaguzi, lakini hatua kwa hatua yalibadilika na kuwa harakati ya umma ambao walitetea uhuru, kupinga ukandamizaji, ubaguzi, ukosefu wa haki na ufisadi.

Mia Mottley, Waziri Mkuu wa Barbados alisema lazima kuhakikisha kwamba taasisi za kimataifa zinazipa nafasi nchi zinazoendelea, hasa nchi ndogo zilizo hatarini au zilizo katika mazingira magumu ya kipato cha kati.

Ilielezwa kuwakwe meza ya kufanya maamuzi ambako nazo zinaweza kuonekana na kusikilizwa ili ziwe mawakala watendaji katika shughuli zao wenyewe na kuongoza miradi ya maendeleo.

Mkutano wa Hadhara Kuu ya Umoja wa Mataifa umeendelea huko NewYork, huku wakuu wa nchi na serikali wakiendelea na juhudi za kutafuta suluhu za changamoto za kimataifa ikiwemo mizozo, ili kuendeleza amani, usalama na maendeleo endelevu.

Ilielezwa kuwa Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani Antony Blinken alikutana na mwenzake wa China Wang Yi mjini New York, wakati Marekani na China zikijitahidi kuleta utulivu katika mahusiano yao yaliyokumbwa na misukosuko.

Mkutano huo unajiri siku chache baada ya Rais wa Marekani Joe Biden kutangaza kwamba China inaiweka Marekani majaribuni kwa sababu ya tabia yake ya kuzidisha uchokozi, hasa katika Bahari ya Kusini ya China na hatua zake kuelekea kisiwa cha Taiwan ambacho Beijing inakichukulia kama himaya yake huku ikishutumu uungaji mkono wa Washington kwa Taipei.

Mwanadiplomasia huyo mkuu wa Marekani alisema ana wasiwasi kuhusu uungaji mkono wa China kwa ulinzi wa Russia na kusisitiza kuwa ni muhimu kuzishinikiza Iran, Korea Kaskazini na China kuacha kuipatia Moscow silaha katika vita vyake na Ukraine. Kuhusu mzozo wa Mashariki ya Kati Blinken alisema Marekani imeweka wazi kuwa inaamini kwamba njia ya kuutatua mzozo huo ni diplomasia na si kuendeleza migogoro.

**DW**

# Makumbusho utamaduni Mnyakyusa kujengwa Rungwe

**Na Grace Mwakalinga**

JAMII ya Wanyakyusa, inatarajia kujenga kituo kikubwa cha makumbusho kitakachosheni vitu mbalimbali vitakavyoelezea historia ya kabila hilo, mila, desturi na utamaduni.

Akizungumza juzi wakati wa kufungua Tamasha la Utamaduni wa Mnyakyusa, linalofanyika litakalofikia tamati leo katika Kijiji cha Makumbusho, Dar es Salaam, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, Patrick Mwalunenge, alisema kituo hicho kinatarajiwa kujengwa wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya.

Mwalunenge alisema Tamasha la Jami ya Wanyakyusa linatoa fursa kujadili na kupeana mbinu za namna ya kujikwamua kiuchumi, kushirikiana katika kuenzi na kudumisha mila na desturi.

"Tamasha hili litukutanisha watu wa jami ya mbalimbali ya kinyakyusa, tunajifunza namna wazee wetu walivyoishi, tunashuhudia ngoma na vyakula vya asili vya kabila letu, hapa ni sehemu inayotuunganisha na wenzetu kutoka maeneo mbalimbali," alisema Mwalunenge.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Tamasha hilo, Enelen Mwakapila, alisema nyumba za asili za kabila hilo, mavazi ya asili, chakula na warsha za namna ya kuenzi utamaduni na kujikwamua kiuchumi.

Alisema licha kufanikisha tamasha hilo, lakini hawana chombo cha kitaifa cha kusimamia maudhui, kupeana elimu kuhusu utamaduni wa Mnyakyusa, kupungua kwa vijana wanaohamasisha kulinda na kuuenzi utamaduni wao.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Makumbusho ya Taifa, Frida Kombe, alisema wataendelea kushirikiana na Jamii ya Wanyakyusa katika kudumisha mila, desturi na utamaduni wao.

Alisema majukumu waliyo nayo ni kutafiti, kuhifadhi na kuelimisha jamii kuhusu urithi wa utamaduni wa asili wa nchi ambao unapatikana kwenye vituo saba vya makumbusho yakiwemo na maeneo 163 ya Malikale.

" Makumbusho ya Taifa ni Taasisi yenye jukumu kukuza na kuendeldeza utamaduni wa makabila yote nchini, tuna simamia program mbalimbali kama vile siku ya utamaduni wa mtanzania ambayo inaratibiwa na Kijiji cha Makumbusho ikiwamo jamii ya Wanyakyusa ambayo leo wanaishehereke a," alisema Kombe.

Mwenyekiti wa machifu kutoka wilaya ya Kyela mkoani Mbeya, Uswege Mwakabululfu, alisema tamasha hilo litasaidia kuondoa dhana potofu ya kudhaniwa machifu ni wachawi.

Alisema kitendo hicho sio cha kweli na jamii inapaswa kuachana na dhana hiyo potofu, akatolea mfano kwamba Rais Samia Suluhu Hassan amewapata thamani machifu kwa kuamua kushirikiana nao kwenye shughuli mbalimbali ikiwemo kulinda na kuenzi mila na desturi za nchi.

Alisema Rais Samia amefanya hivyo kwa sababu ametambua mchango wa machifu nchini kwamba ni watu wanaolisaidia Taifa katika kukabiliana na masuala mbalimbali yanayokwenda kinyume na maadili.

# Naibu Waziri awataka wazazi kutimiza wajibu

**Na Lusungu Helela**



NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deus Sangu (pichani), amewataka wazazi kutimiza jukumu la malezi ya watoto badala ya kuwaachia walimu pekee yao.

Sangu amesema malezi ya wazazi kwa watoto ni muhimu sana katika nyakati hizi kutokana na wimbi kubwa la mmonyoko wa maadili linaloikumba jamii.

Aliyasema hayo juzi katika mahafali ya 37 ya kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Kibakwe, Mpwapwa mkoani Dodoma.

Nauibu Waziri Sangu alisema kitendo cha wanafunzi 80 kati ya 247 kuacha shule walioanza kidato cha kwanza mwaka 2021 kutokana na sababu za utoro na mimba, kinaonyesha kuwa kuna baadhi ya wazazi hawawajibiki ipasavyo

" Leo (juzi) watoto 157 wanahitimu kidato cha nne huku tukiwa tumepoteza watoto 80 kutokana na utoro na mimba za ututoni, hii si sawa, wazazi liangalieni hili," alisisitiza Sangu.

"Elimu ndiyo msingi wa kila kitu. Ukiamua kuwa mfanyabiashara ni lazima uwe na elimu. Ukitaka kuwa mjasiliamali ni lazima uwe na elimu ndiyo maana Rais Dk. Samia Suluhu Hassan anahakikisha watoto wote wanapata elimu bila ubaguzi wowote," aliongeza.

Kutokana na hali hiyo, Sangu aliwataka wazazi kujiepusha na tabia ya kuwaozesha mabinti katika umri mdogo badala yake wahakikishe wanakumbatia elimu itakayowaandaa kwa ajili ya kupambana na maisha

Katika hatua nyingine, Sangu alisema serikali inatarajia kuwapangia vituo vya kazi walimu 247 katika Mkoa wa Dodoma hususan katika wilaya ya Mpwapwa kutokana na uhaba mkubwa wa walimu unaoikumba wilaya hiyo

Alisema walimu hao watapelekwa katika wilaya mbalimbali ikiwamo Mpwapwa hivi karibu ikiwa ni kati ya ajira 11,015 za walimu zilizokuwa zimetangazwa na Ofisi ya Rais, Sekretariet ya Ajira, Julai, mwaka huu.

Alisema serikali imejipambanua kwa kuhakikisha watoto wanapata elimu bora ndiyo maana inafanya kila liwezekanalo kupambana na uhaba wa walimu katika shule mbalimbali nchini na hatimaye kuwa kuwa historia.

Aidha, Sangu aliipongeza shule hiyo kwa mikakati ya kufuta daraja la nne na sifuri na kufanikiwa kwa hali ya juu jambo ambalo kwa miaka miwili iliyopita hakuna waliopata daraja la nne na sifuri

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Kisa cha Urafiki Jazz kutunga wimbo Asmaha



**Na Adam Fungamwango**

Jamaa anaendelea kumwambia mpenzi wake kuwa ayashike maneno aliyomwambia kuwa mbali na wambea na wafitini ili mapenzi yao yafanikiwe, wakishafanikiwa kuwashinda wafunge ndoa.

SAFARI yetu ndefu ha, mimi na wewe, Asmaha mpenzi wa moyo wangu, tumezungukwa na madhoruba mengi sana. Tumuombe Mola atulinde tuwe salama, wimbi la mapenzi limetupata mimi na wewe, na tujitahidi kulikabili tuwe salama."

Hiki ni kipande cha mashairi ya wimbo uitwao 'Asmaha', uliorekodiwa miaka ya mwanzo ya 1980 na bendi iliyokuwa ikimilikiwa na kiwanda cha kutengeneza nguo cha Urafiki.

Bendi yenyewe iliitwa Urafiki Jazz. Kiwanda hicho kilijengwa kwa ushirikiano kati ya Tanzania na China, urafiki wa nchi hizi mbili ndio uliosababisha kiwanda kipewe jina hilo na hata bendi ya muziki wa dansi.

Maudhui wa wimbo huo ni wa mapenzi lakini ni tahadhari inayotoka kwa mwanamume, akimwambia mpenzi wake awe na tahadhari na watu wabaya kwenye penzi lao.

Hata hivyo mwanamume anaongea na mpenzi wake kwa lugha ya picha, haelezi moja kwa moja, badala yake anatumia maneno kuwa wamezungukwa na madhoruba mengi. Hawako baharini hao, ila wapo kwenye mapenzi.

"Asmaha oooh Asmaha, wewe ndiwe ua la rohoni mwangu. Asmaha oooh Asmaha, wewe ndiwe ua la rohoni mwangu.

Nakuomba ushike maneno haya, ili mapenzi yetu yafanikiwe, tukijaliwa tupate funga ndoa yetu, oooh Asmaha, oooh Asmaha wa moyo.

Asmaha oooh Asmaha, wewe ndiwe ua la rohoni mwangu. Asmaha oooh Asmaha, wewe ndiwe ua la rohoni mwangu."

Jamaa anaendelea kumwambia mpenzi wake kuwa ayashike maneno aliyomwambia kuwa mbali na wambea na wafitini ili mapenzi yao yafanikiwe, wakishafanikiwa kuwashinda wafunge ndoa.

Ni mashairi machache sana yaliyomo kwenye wimbo huu, lakini yana uzito mkubwa mno kama jabali.

Ni maneno ambayo watu wawili wapendanao wakitaka penzi lao lifanikiwa ni lazima wafuate hayo, vinginevyo penzi halitadumu.

Siku zote penzi bora ni lile lenye wafitini wengi. Ukiona watu wameliacha tu penzi la watu fulani wawili ujue hawavutiwi nalo. Na hawana chochote cha kuwashughulisha watu. Hawaonei kijicho wala wivu. Lakini ukiona watu walifuatafuata sana penzi wa la watu fulani ujue linawauma na kuwakereketa, hivyo wanachotaka ni kulivunja tu na si kuliendeleza. Waendelezaji wa penzi ni wenyewe tu wawili wakisikilizana.

Wimbo huu ulitungwa na kiongozi wa bendi ya Urafiki Jazz, Juma Mrisho, 'Ngulimba wa Ngulimba.'

Ni wimbo wa tukio la kweli kama ilivyo kwa nyimbo nyingi za zamani. Huyu dada Asmaha aliyemwimba baadaye akaja kuwa mkewe.

Bendi ya Urafiki ilikuwa ziarani Tanga. Wakati Ngulimba akiwa nje ya hoteli waliofikia na mpiga solo wale, Michael Vincent, walipita mabinti wawili warembo ambao waliwastua wanamuziki hao.

Wakawasalimia na kuwauliza majina yao. Mmoja akajitaja kwa jina la Asmaha. Ngulimba akavutiwa naye, Vicent akavutiwa na yule dada mwingine.

Wajitambulisha kuwa wao ni wanamuziki na watapiga kwenye ukumbi wa Tangamano siku ile usiku. Wakawaalika, nao wakasema watakuja.

Walipoondoka haraka Ngulimba alianza kutunga mashairi ya wimbo kulizunguka na kulitaja jina la mwanadada yule aliyempenda. Akaanza mazoezi na mwenzake Vincent hapo hapo.

Baadaye wakawaita wanamuziki wote na kuufanyia kazi wimbo wa mgeni yule atakayefika kwenye onyesho.

Saa sita usiku wakati dansi likiendelea, Ngulimba akiwa na wasiwasi kuchelewa kwa mgeni wake, ghafla waliowaona warembo wale wawili wakiingia, wakiwa wamejipamba kama malaika.

Muziki ukazimwa na wimbo huo 'Asmaha' ukapigwa. Binti hakuamini macho na masikio yake. Kutungiwa wimbo na bendi kubwa kama ile kwa heshima yake, lilikuwa ni jambo ambalo hakutegemea.

Ngulimba hakuhitaji kujieleza sana, kilichotokea hapo ilikuwa tayari ishara tosha ya kumhitaji. Na kweli wakawa wapenzi na baadaye wakaona.

**Tume meseji 0716 350534**

# HADITHI

# Nyuma ya Pazia-2

TAARIFA za habari kwenye televisheni, redio, mitandao ya kijamii zinaarifu kutekwa kwa mtoto wa miaka sita, Macaire, mwanafunzi wa darasa la kwanza katika shule moja Mbezi Dar es Salaam. Mashuhuda wanasema alinyakuliwa na mwanamume mmoja aliyeshiba, kujaa misuli na kukimbilia kwenye gari lililokuwa pembeni mwa barabara ya Bagamoyo, Dar es salaam, ambalo mlango wake ulikuwa wazi. Wazazi wa mtoto wanapigiwa simu na watekaji wakitaka kiasi cha Sh. Milioni 15 ili wamwachie. Jeshi la Polisi linaingia kazini kumsaka au kuwasaka watekaji. Walichogundua ni kisa cha kushangaza, kusisimua ambacho utakipata utakaposoma kila aina ya nakala ya gazeti hili, ili kuupata mkasa mzima wa tukio.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

NAJUA kuwa mkeo mlitengena muda mrefu, ndiyo maana kwenye mikutano unakuja wewe, mama yake anakuja mara chache sana, kwa maana hiyo nimempigia pia mzazi mwenzako naye nadhani anaweza kuwasili mida hii hii, maana kaniambia anakuja, inawezekana foleni tu imemchelewesha." "Ni kweli, kuna foleni sana, mimi mwenyewe niliamua kushuka kwenye daladala na kuchukua bodaboda ili nifike haraka." Macky aliongea kwa unyonge. "Vipi unamsubiri?" Mwalimu akauliza. "Hapana hata nguvu ya kumsubiri mtu hapa sina. Halafu unajua watoto wa kike, atakuja analia hapa halafu tuanze kazi ya kubembeleza tena badala ya kufikiri nini kitafanyika. Tena imekuwa vizuri sana mimi nimekuja kabla yake." Akasema Macky huku akinyanyuka.

"Basi Mwalimu kesho tutakutana kituo cha polisi mjini." "Tuombe Mungu."

Walitoka nje ya ofisi na kwa sababu hapakuwa mbali sana na barabara, mwalimu alimpeleka hadi kituoni, huku akimpa maneno ya faraja kuwa hakuna baya lolote litakalomfika mtoto.

"Nashukuru, tuendelee kuomba Mungu, ila mwalimu simu yangu ipo wazi hata usiku wa maanani, lolote litakalotokea utanipigia." "Haina neno, we nenda kampumzike."

Baada ya kuhakikisha amepata usafiri, mwalimu Kisanga akarejea ofisini kwake haraka kwani alitegemea kupata ugeni mwingine wa mama mzazi wa Macaire baada ya baba yake kuondoka. Na kweli alipofika nje ya ofisi yake alimuona mwanamke ambaye alionekana analia akiwa ameshikiliwa na mwanamume mwingine. Wala haikuhitaji kuuliza kama yule ndiye mama Macaire.

Alionekana bado mwanamke mbichi tu kuanzia miaka 25 mpaka 28 hivi.

Alikuwa amevaa dela lenye rangi nyingi tofauti na kiunoni akiwa amefunga khanga. Ile ilimthibitishia mwalimu Kisanga kuwa mama huyo alikuwa amelia sana mpaka ameamua kufunga khanga kiunoni. Hili hufanywa na kinamama katika matukio maalum tu.

Wakati akipata jambo baya la huzuni au msiba, au wakati mwingine hata akipata hasira na kwenda kumpa aliyemkera makavu, kama kumsuta.




**"Mama mwanangu, mama mwanangu miee, jamani, nitamuona tena wapi mimi Macaire.." Alilia na kuombolewa huku akitetemeka na kutikisika kama mtu anayetaka kuruka.**

Mwanamume aliyemshika, alifanya hivyo kutokana na mwanamke huyo kuonekana kuishiwa nguvu.

"Mama mwanangu, mama mwanangu miee, jamani, nitamuona tena wapi mimi Macaire.." Alilia na kuombolewa huku akitetemeka na kutikisika kama mtu anayetaka kuruka.

Mwalimu Kisanga alipofika akaanza kwa kusema, "karibuni ofisini", ili waliokuja wajue mtu waliyemfuata ni yeye. Vinginevyo wangemshangaa tu. Alichotaka kumsaidia mwanamume yule kumuingiza mama Macaire ofisini.

Walimshika na kumtembeza taratibu baada ya kuonekana anaishiwa nguvu, mwisho wake akamuweka kwenye kochi. Aliendelea kulia na kuomboleza. Ilibidi sasa mwalimu Kisanga aanze kuongea na mtu aliyekuja naye.

Angalau alikuwa anamfahamu mama Macaire kwani mara chache sana huwa anakuja shuleni kuongea na mtoto wake, lakini aliyefuatana naye hamfahamu.

Alikuwa ni mwanamume mkubwa kwa umri kuliko baba Macaire aliyeondoka punde. Alionekana pia ana uwezo kidogo kuliko aliyeondoka. "Unaitwa nani?" "Naitwa Zabron." "Okay, ukoje naye mama Macaire?" Akasita kidogo, halafu akajibu "Ninaishi naye kwa sasa, ila natarajia kumuoa kabisa awe mke wangu wa ndoa hivi karibuni." Mwalimu hakutaka kuingia kwa undani sana na si lengo lake hilo, bali alitaka kutoa habari kwa mtu ambaye ni mtu wa karibu na mama Macaire kwa sababu alivyoonekana hata kama atasikia, lakini kuna mengine yanaweza kumpita kutokana na majonzi na mawazo.

"Okay, sasa ni hivi. Ilikuwa ni saa 9:00 hivi alasiri, gari moja lilipaki karibu na basi letu na shule pamoja na geti. Basi lilikuwa nje, wanafunzi walifungua geti ili wapande kwa ajili ya kuwarudisha makwao. Kwa bahati mbaya sana, kuna mtu mmoja alitoka kwenye gari na kumteka kijana wetu Macaire."

Sauti kali kutoka kwa mama Macaire ilisikika. Mwanzo alilia taratibu, lakini aliposikia maneno ya mwalimu alilia kwa sauti kubwa kama vile ndiyo taarifa hiyo anaisikia kwa mara ya kwanza, au kapata habari ya msiba.

Mwalimu Kisanga alinyanyuka na kumfuata mama Macaire kitini, akampiga begani na kumbembeleza.

"Unasikia mama Macaire, tumeshapiga ripoti polisi, na wameshaanza uchunguzi kwa hiyo usilie wala usihuzunike sana..." "Mwalimu huwezi kujua mtoto wamteka kwa sababu gani hawa, mimi sina imani kabisa, wameshamuua masikini mtoto wangu, mtoto mwenyewe ndiyo huyo huyo mmoja, Macaire wangu uko wapi saa hizi baba, wamekutesa? Wamekupa chakula? Au wamekuua..." "Usiseme hivyo, hapa kinachotakiwa ni kusubiri na kumuomba Mungu," mwalimu Kisanga alizidi kumpoza. Baadaye sauti ilipungua na akabaki na kwikwi.

"Bwana Zabron, hiyo ndiyo habari na huyu mwenzako, nadhani hata wewe sasa linakuhusu hili, tunatakiwa tuwe Makao Makuu ya Jeshi la Polisi Kanda, majira ya saa 2:00 asubuhi kesho. Naomba umlete mwenzako, ili tujue wanasemaje." " Sawa mwalimu, nitamleta." Mlio wa gari ulisikika na ikaonyesha limesimama nje ya shule hiyo. "Nimeita gari kwa njia ya mtandao." Zabron alisema ili kumtoa mashaka mwalimu ambaye alionekana kutaka kufuatilia kwa nini limesimama ghafla hapo. Wote wawili wakasaidia kumnyanyua mama Macaire na kumuweka ndani ya gari, wakaagana.

**********************************

Simu yake ya mkononi iliita. Aliingiza mkono mfukoni na kuangalia ni nani anapiga. Hakumjua kwani haikuseviwa. Ina maana namba ilikuwa ngeni. Wasiwasi ukamjia. Akabonyeza kitufe cha kufungulia sauti huku mikono ikiwa inatetemeka. "Ni nini? Ni nani huyu? Macaire amepatikana au..." Akawa anajiuliza maswali. jasho lilikuwa linamtoka na nguvu zikamwisha. Akaamua kukaa kwenye kochi, kwani mwazo alikuwa amesimama.

"Nadhani wewe ndiyo Macky Macaire." "Ndi Ndi Ndiyo mimi." Akajibu kwa woga na sauti ya kutetemeka.

"Vipi mbona hujiamini?" Sauti nzito iliyotulia ilimuuliza baada ya kugundua mpokeaji alikuwa ana kitete.

Macky alishindwa ajibu vipi. Akabaki kimya. Lakini hapo hapo akili ikamjia, akamuuliza aliyempigia.

"Kwani wewe nani mwenzangu?" Badala ya kujibu kikafutia kicheko kifupi cha dharau. "Huna haja ya kujua jina langu na wala haitokusaidia chochote kwa sasa." Ilijibu sauti hiyo kwenye simu kwa kujiamini.

"Tusipoteze sana muda, lengo la kukupigia ni kukutaarufu kuwa mtoto wake Macaire Macky tunaye sisi.

Yupo salama salimini na anaweza kuongea naye ukitaka. Ila uhai wake unaweza ukakatika baada ya wiki moja. Ili tusimuue, unapaswa utoe shilingi milioni 15, utampata akiwa hai bila hata mikwaruzo." Ilikuwa ni habari mpya kwa Macky.

Kwanza alichofurahi ni kusikia mtoto wake yu hai, licha ya kwamba hajamsikia sauti. Ila kilichomuacha hoi ni kutakiwa atoe kiasi hicho cha pesa ambacho ni kingi sana kwake.

**Itaendelea Jumapili**



# LUKAMBA HARUDI TENA KWA DIAMOND

MSANII na mpiga picha wa zamani wa Diamond Platnumz, Lukamba, amesema anamkubali sana sana na yeye ndiyo 'role model' wake kwani amejifunza mengi sana kutoka kwake, lakini hawezi tena kurudi kwake na kuwa pamoja.

Lukamba amesema kwa sasa anaona nchini hakuna msanii bora kama Diamond, lakini akitoka huyo anafuata yeye kwani amejifunza mengi kutoka kwake, hivyo wanafanana kwa mambo mengi, huku akijitabiria makubwa siku za mbele.

"Nampenda sana Diamond, ndiye 'role model' wangu kwenye muziki maana nimejifunza mengi kutoka kwake, na mimi naweza kusema ndiyo namba mbili akitoka yeye, hivi sasa nchini hakuna msanii anayemshinda kwa chochote, muziki, uchumi hata kusafiri sana, naamini na mimi huko mbele ya safari, nitakuwa kama Diamond na Afrika nzima itanijua. Lakini pamoja na hayo yote siwezi kurudi kufanya naye kazi, kwa sasa nafanya muziki wangu mwenyewe binafsi," alisema Lukamba.

# NAOMI PESA UNACHEZEA VIKOBA?


Mwanamitindo maarufu wa Uingereza, Naomi Campbell ameondolewa kwenye nafasi udhamini wa shirika la hisani kwa miaka mitano baada ya Tume ya Misaada ya Uingereza kugundua ubadhirifu mkubwa wa fedha katika shirika hilo alilolianzisha.

Uchunguzi wa Tume ya Misaada ya Uingereza uligundua kuwa kati ya Aprili 2016 na Julai 2022, asilimia 8.5 ya matumizi ya jumla ya hayakuwa sahihi.

Hii ilijumuisha kutumia pesa za usaidizi kulipia malazi ya Campbell katika hoteli ya nyota tano huko Cannes, Ufaransa, jambo ambalo mdhibiti aliona ulikuwa ni ufujaji wa fedha.

Inadaiwa alitumia paundi 9,400 za fedha za shirika hilo kwa kukaa kwa siku tatu katika hoteli ya nyota tano huko Cannes, Ufaransa.

Fashion for Relief ilianzishwa na Campbell mwaka wa 2005 kwa lengo la kuunganisha tasnia ya mitindo ili kuondoa umaskini na kuendeleza afya na elimu, kwa kutoa ruzuku kwa mashirika mengine na kutoa msaada kwenye majanga ya kimataifa.



## ZISIKUPITE

### SOUTHGATE NA EVERTON

MMILIKI mtarajiwa wa Everton, Dan Friedkin amemtambua kocha wa timu ya taifa ya England, Gareth Southgate mwenye umri wa miaka 54, kama mtu anayetarajiwa kuchukua nafasi ya Muingereza mwenzake Sean Dyche mwenye miaka 53, katika uwanja wa Goodison Park. **(GiveMeSport)**

### LIVERPOOL YASAKA NYOTA

LIVERPOOL inajiandaa kuivamia Bayer Leverkusen kwa kiungo wao wa Ujerumani, Florian Wirtz mwenye umri wa 21, mlinzi wa Uholanzi Jeremie Frimpong mwenye miaka 23, na kiungo wa kati wa Argentina Exequiel Palacios mwenye miaka 25. **(CaughtOffside)**

### LIVERPOOL YAMTAKA ZUBIMENDI

LIVERPOOL pia wana nia ya kumsajili kiungo wa Hispania, Martin Zubimendi mwenye umri wa miaka 25, kutoka Real Sociedad katika msimu wa Januari wa usajili wa wachezaji **(Fabrizio Romano)**

### GOMEZ AWA LULU EPL

MLINZI wa Liverpool na England, Joe Gomez mwenye umri wa miaka 27, anawaniwa na klabu za Aston Villa na Newcastle United. **(Football Insider)**

### MURILLO ATAKIWA MADRID

REAL Madrid inamfuatilia mlinzi wa Nottingham Forest, Murillo mwenye umri wa miaka 22, lakini wanakabiliwa na ushindani kutoka Barcelona na Bayern Munich kumpata Mbrazil huyo. **(HITC)**

### UNITED YAMTAKA GOMEZ

KLABU za Newcastle United, Manchester United na Tottenham Hotspur ni miongoni mwa klabu zinazovutiwa na kiungo wa kati wa Lille na England, Angel Gomes mwenye umri wa miaka 24. **(GiveMeSport)**

### BARCA YAPAMBANA KWA KIPA

BARCELONA itarajiwa kufanya mazungumzo ya dharura wiki hii kujadili iwapo watamleta golikipa mpya kuchukua nafasi ya mchezaji wao wa kimataifa wa Ujerumani aliyejeruhiwa Marc-Andre ter Stegen. **(ESPN)**

### DIAZ KUONGEZA MKATABA

LIVERPOOL inatarajiwa kufanya mazungumzo na winga wa Colombia Luis Diaz mwenye umri wa miaka 27, kuhusu mpango wa kuongeza mkataba wake hadi 2027 kufuatia mwanzo wake mzuri wa msimu huu. **(Football Insider)**

### HUGO LARSSON AFUATILIWA

KLABU kadhaa zinamfuatilia winga wa Eintracht Frankfurt aliye na umri wa miaka 20 kutoka Sweden, Hugo Larsson. **(Fabrizio Romano)**

### SPURES KUMSHAWISHI DIBLING

KLABU ya Southampton inatumaini kumshawishi kiungo wa kati wa England, Tyler Dibling mwenye umri wa miaka 18, kusaini mkataba mpya huku Manchester United wakionesha nia ya kutaka kumnunua. **(GiveMeSport)**

### CONNOLLY KUTUA BRIGHTON

KLABU ya Sunderland inatazamia kumsajili mshambuliaji wa zamani wa Brighton na Jamhuri ya Ireland, Aaron Connolly mwenye umri wa miaka 24, kutoka Hull City. **(Sun)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# SOLSKJAER: MAN UTD ILIFANYA MAKOSA KUMREJESHA RONALDO

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa zamani wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer amekiri kuwa klabu hiyo ilifanya makosa kwa kumsajili tena Cristiano Ronaldo mwaka 2021.

United walipata fursa ya kuungana tena na mshindi huyo mara tano Ballon d'Or ilipoonekana kana kwamba angeondoka Juventus kwenda Manchester City, na Ronaldo alifurahia mafanikio mengi ya mapema chini ya Solskjaer na bosi wa muda Ralf Rangnick.

Ronaldo alifunga mabao 24 katika mechi 38 katika michuano yote katika msimu wake wa kwanza nyuma, lakini haraka akapoteza nafasi yake kufuatia kuwasili kwa kocha mpya Erik ten Hag.

**Amebainisha kuwa kurejea kwa nyota huyo wa Ureno kulibadilisha ......**

**Wawili hao hawakuiva lilipelekea Ronaldo kuondoka kwenda Al Nassr Januari 2023.**

Alipoulizwa iwapo alikuwa na majuto yoyote kuhusu kumsajili tena Ronaldo, Solskjaer aliambia Jukwaa la Biashara la Oslo: "Ili kujibu hilo, muktadha mdogo unahitajika. Cristiano Ronaldo, mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani kwa miaka 15 iliyopita.

"Kwa hiyo kuwasili tena wa Cristiano kuliathiri chumba kizima cha kubadilishia nguo, nguvu kwenye chumba cha kubadilishia nguo. Labda wachezaji wengine walijiona sio muhimu kwa sababu huyu ni mmoja wa mastaa wa dunia.

"Alifanya vizuri. Alikuwa mfungaji bora mwaka huo, alifunga mabao 24 au kitu, lakini sikuwa na kazi wiki kumi baadaye!

Solskjaer hajafanya kazi kama kocha tangu kuondoka kwake kutoka United mnamo Novemba 2021 lakini alikiri kuwa angependa kuwa bosi wa timu ya taifa ya Norway, huku akikiri angeruka nafasi hiyo kurejea United.

# GUARDIOLA AJIBU TUHUMA ZA ARTETA



**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amejibu madai ya Mikel Arteta kwamba ana habari za ndani kuhusu Manchester City kwa kumwambia kocha huyo wa Arsenal ajieleze.

Arteta aliulizwa Jumanne kujibu malalamiko ya wachezaji wa City kuhusu matumizi ya Arsenal ya "sanaa ya giza" wakati wa mchezo wao ulioishia kwa sare ya 2-2 kwenye Uwanja wa Etihad.

Arteta ambaye alikuwa msaidizi wa Guardiola pale Etihad kati ya mwaka 2016 na 2019, alitoa jibu lisiloeleweka, akisema: "Nilikuwa huko kwa miaka minne. Nina taarifa zote, niamini."

Dhana ilikuwa kwamba Arteta anajua City pia inatumia mbinu zilezile, lakini nukuu hizo zilipotolewa kwa Guardiola, alisema mwenzake anapaswa kuwa "wazi zaidi."

"Wakati ujao anapaswa kuwa wazi zaidi inamaanisha nini? Alisema alikuwa hapa kwa miaka minne na tunajua hasa kilichotokea hapa, kwa sababu inaweza kuhusishwa katika mchakato wote sasa na mashtaka 115; labda ni kuhusu hilo. anajua habari kuhusu hilo labda.

"Natumaini swali hili limeulizwa. Anaweza kujibu hasa maana yake aliposema alikuwa hapa na anajua kinachotokea hapa."

Uhusiano kati ya klabu hizo mbili umedorora huku zikipambana kwa ajili ya taji la Ligi Kuu England, ingawa Arteta alisema katika mkutano wake na waandishi wa habari Ijumaa kwamba ushindani huo hautaathiri uhusiano wa kibinafsi kati ya makocha hao wawili.

# Martínez afungiwa na FIFA

**LONDON,** England

GOLIKIPA wa Argentina, Emiliano "Dibu" Martínez amesimamishwa na kamati ya nidhamu ya FIFA kwa mechi mbili baada ya kubainika kuwa alionesha tabia ya kuudhi na "kukiuka kanuni za uchezaji wa haki."

Atakosa mechi ya Argentina ya kufuzu Kombe la Dunia dhidi ya Venezuela Oktoba 10 na Bolivia Oktoba 15.

FIFA iligundua kuwa Martínez alikiuka kanuni zake za maadili alipokuwa ameshikilia mfano wa kombe la Copa America kwenye eneo la paja lake, akimaanisha sherehe aliyofanya kwenye Kombe la Dunia la FIFA la 2022, baada ya ushindi dhidi ya Chile Septemba 5.



Nyota huyo wa Aston Villa pia aliadhibiwa kwa kitendo chake kufuatia kichapo cha 2-1 cha Argentina dhidi ya Colombia Septemba 10, wakati wa kusukuma vifaa vya operator wa kamera baada ya filimbi ya mwisho.

Opereta, Jhonny Jackson aliviambia vyombo vya habari vya Colombia kwamba "alishambuliwa" na Martínez, akisema "alihisi hasira sana."

Shirikisho la Soka la Argentina (AFA) lilisema utetezi uliwasilishwa na mchezaji na chama kabla ya FIFA kuthibitisha adhabu hiyo.

La Albiceleste hao kwa sasa wanaongoza msimamo wa kufuzu kwa Kombe la Dunia wakiwa na pointi 18 katika mechi nane, pointi mbili zaidi ya Colombia walio nafasi ya pili.

# Ange: Son hatakiwi kuchezea mechi nyingi

**LONDON,** England

ANGE Postecoglou amesema kuwa sio jambo jema kwa Son Heung-Min kushiriki katika kila mechi ya Tottenham Hotspur msimu huu na kwamba fowadi huyo tayari amecheza zaidi ya ilivyopangwa hapo awali katika wiki za mwanzo za msimu Huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 alichechemea kutoka uwanjani baada ya kupata matibabu dakika ya 71 ya ushindi wa Spurs kwenye Ligi ya Europa dhidi ya Qarabag siku ya Alhamisi.

Son ameichezea Spurs mechi 415 katika michuano yote tangu asajiliwe na klabu hiyo mwaka 2015 na ameshiriki katika kila mechi msimu huu, ikijumuisha ushindi wa raundi ya tatu wa Kombe la Carabao dhidi ya Coventry City mnamo Septemba 18.

Siku ya Jumatano, Son alizungumza dhidi ya wingi wa michezo ambayo wanasoka sasa wanapaswa kucheza, akisema kwamba "wakati mwingine ni ngumu sana" na kwamba "hatari ya kuumia ni kubwa."

Alipoulizwa kama ni "endelevu" kwa Son kuendelea kuichezea Spurs dakika nyingi akiwa na umri wa miaka 32, Postecoglou alisema: "Hapana, hapana ... ningetaka kupunguza aina yake ya kazi katika sehemu hii ya mapema ya mwaka.

"Lakini tulipoteza kutokana na jeraha la Richarlison, kisha tukampoteza Dominic Solanke, kisha tukampoteza Wilson Odobert.

"Na wazo, kama nilivyosema, la kusaini Dom na kumleta Wilson na kuongeza mkopo wa Timo Werner lilikuwa kwamba tunaweza kusimamia mzigo wake kwa sababu ana soka la kimataifa pia. Ni jambo ambalo ninakumbuka ni tu. hali hadi sasa Na Sonny anataka kucheza. Huo ni mtazamo wake, lakini lazima tuwe na busara kuhusu hilo.

"Sidhani kama ni lazima kufanya mengi na umri wake. Sijaona hilo likimuathiri. Zaidi ya hayo, sidhani kama aina ya kazi katika mchezo wa kisasa ni endelevu. Tumezungumza moja kwa moja. mengi kuhusu upakiaji mwingi wa mechi, nadhani nilisema wiki iliyopita kwamba sehemu ya jukumu hilo nadhani iko kwetu, wakati kalenda iko hivi, kujaribu kuwalinda wachezaji wetu na bila shaka tukiwa na Sonny itabidi tuwe waangalifu. yake."

Postecoglou alikiri kwamba ingawa Son anataka kucheza michezo mingi iwezekanavyo, hafikirii kuwa anahitaji kukaa chini na nahodha wake kuelezea maamuzi yake.

HABARI MICHEZO

# BAO LAMPA 'KIBURI' BACCA, ATAKA KIATU CHA DHAHABU

Na Adam Fungamwango

BAO alilofunga Jumatano iliyopita kwenye Uwanja wa Sokoine Mbeya dhidi ya KenGold, limempa kiburi beki wa kati wa Yanga, Ibrahim Hamad 'Bacca', akisema ndoto yake sasa ni kuwa na mwendelezo wa kufunga mabao kwa ajili ya kusaka ufungaji bora wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Bacca, alisema bao alilofunga dhidi ya KenGold limempa chachu ya kuendela kupachika mabao, hivyo kuwataka mastraika wa Ligi Kuu kuwa makini, kwani ameingia rasmi kwenye mapambano ya kuwania kiatu.

"Lile bao limeniamsha, tayari nimeshaanza kuona inawezekana kabisa kupambania ufungaji bora, na ni malengo yangu siku moja kuwa beki ninayefukuzana na mastraika kuwania kiatu, ikiwezekana nikipate kabisa ingawa najua si rahisi.

Kwa ligi yetu hii ukifikisha mabao 15 tu tayari mfungaji bora, nawaambia kina Prince Dube na wenzake, safari hii na mimi nipo, wacha tuone," alisema beki huyo.

Lilikuwa ni bao pekee kwenye mchezo huo, Yanga ikishinda bao 1-0, lakini pia ni la kwanza kwa beki huyo tangu alipojiunga na Yanga 2022, akitokea KMKM ya Zanzibar, na kuongezewa mkataba mpya mwaka jana unaomuweka Jangwani hadi mwaka 2027.

"Najisikia furaha sana kufunga bao langu la kwanza nikiwa Yanga, nataka kuwa na mwendelezo sasa wa kufunga, nimeona raha ya kupachika mabao nitakuwa najituma zaidi ili niendelee kufunga.

Nadhani mpaka sasa kwenye orodha ya wafungaji hakuna aliyefikisha mabao matano na kama ndiyo hivyo ngoja niongeze nguvu ya kupambania kiatu mwisho wa msimu," alisema.

Aidha, alisema kinachompa nguvu hiyo ni jinsi walivyojifunza mazoezini kumalizia mipira ya adhabu kwa wapinzani, hivyo anaona atafunga sana.

"Nilivyofunga mimi lile bao siyo kama ilikuwa bahati, tulifanya mazoezi jinsi ya kupiga mipira ya faulo na kufunga na hasa sisi mabeki unajua tumezoea sana mara kwa mara kuruka, hivyo inakuwa rahisi kwenda juu kuuwania mpira,

Kwa maana hiyo wala sikushangaa nilipofunga kwa sababu tulijua itatokea tu kama siyo kwenye mchezo ule, basi mwingine, na utakuwa ni mwendelezo wetu," alisema beki huyo

MAGONGO...



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Lumumba (jezi nyeupe) na wanafunzi wa Shule ya Msingi Yuniti ya Ukonga jijini Dar es Salaam wakiwania mpira wakati walipokuwa wakicheza mchezo wa magongo katika mashindano kwa shule za msingi na Sekondari yaliyofanyika kwenye viwanja vya Jakaya Kikwete jana. **PICHA:JUMANNE JUMA**

# Ngorongoro yaahidi kulibakisha kombe la CECAFA U-20 nyumbani

Na Adam Fungamwango

WAKATI michuano ya Kombe la Afrika Mashariki na Kati chini ya miaka 20 ikitarajiwa kufanyika Tanzania Oktoba 6 mwaka huu, Kocha Mkuu wa Ngorongoro Heroes, Charles Mkwasa, amesema kwa maandalizi aliyoyafanya anaimani watafanya vyema, ikiwemo kubakisha ubingwa huo hapa nchini.

Akizungumza wakayi wa mazoezi ya timu hiyo, Uwanja wa KMC Complex, Mwenge, Dar es Salaam, Mkwasa, amesema anafurahi kuona vijana wake wanapambana sana kwenye mazoezi, hivyo kumpa uwanda mpana wa kuchagua kikosi bora cha mwisho kabla ya michuano kuanza.

"Vijana wanapambana sana, wapo vizuri, tunaendelea na mazoezi kwa ajili ya kuchuja kikosi, tuko asilimia kama 70 hivi tunaangalia, ila kwa sasa tutahitaji mchezo mmoja wa kirafiki, kabla ya kuanza mashindano, nimeridhika na maendeleo ya kikosi changu, nadhani mpaka michuano ianze tutakuwa fiti na tutafanya vyema kwenye mashindano haya, hata kutwaa ubingwa," alisema Mkwasa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Shirikisho la Vyama vya Mpira wa Miguu Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), timu ya taifa ya Tanzania chini ya umri huo, itacheza Oktoba 6 dhidi ya Kenya kwenye Uwanja wa KMC Complex, ambapo kabla ya hapo, kutakuwa na mchezo kati ya Sudan dhidi ya Djibouti.

Taarifa hiyo imesema kuwa michuano hiyo itachezwa kwenye makundi mawili, ambapo Kundi A litakuwa na timu za Djibouti, Kenya, Rwanda, Sudan na Tanzania, huku Kundi B litauiwa na timu za Burundi, Ethiopia, Sudan Kusini na Uganda.

Timu mbili za kwanza kwenye kila kundi zitacheza nusu fainali, Oktoba 18, kabla ya fainali kupigwa Oktoba 20.

Mara ya mwisho michuano hiyo ilichezwa 2022 nchini Sudan, ambapo Uganda ilitwaa ubingwa kwa kuichapa Sudan Kusini mabao 2-1, mechi iliyopigwa Novemba 11, Uwanja wa Al Hilal nchini humo, Tanzania ikiishia hatua za makundi

## Yanga vitani Dar, Simba Dodoma

INATOKA UK. 24

waje kutusapoti, waje kuwashangilia wachezaji wao na kutusaidia kupata ushindi," alisema Fadlu, raia wa Afrika Kusini.

Kocha Mkuu wa Dodoma Jiji, Macky Maxime, amesema wamejipanga kucheza dhidi ya Simba, huku wakijua wanacheza na timu kubwa.

"Tunacheza na Simba, lakini nimeandaa vijana wangu nadhani tutawakabili vizuri na mchezo utakuwa mzuri pia," alisema.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Moses Mpunga, amewataka mashabiki wa Simba kutokwenda na matokeo uwanjani.

"Moja kati ya viwanja vigumu kwa Simba ni hiki cha Jamhuri Dodoma, huwa wanashinda lakini kwa tabu sana, wanashinda bao moja moja katika mazingira magumu, lakini nadhani safari hii hawachomoki," alisema.

Katika mchezo utakaopigwa Chamazi usiku, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema wamejiandaa vyema na mchezo huo, lakini akienda kwa tahadhari kwani anakwenda kucheza na mpinzani bora.

"Tunakwenda kucheza mchezo dhidi ya mpinzani mgumu, huwa nasema siku zote michezo hii siyo rahisi, inabidi tuwaheshimu pia wapinzani wetu. Nimeifuatiliwa msimu huu, KMC ni timu ngumu, na Ligi Kuu Tanzania kila msimu unakuwa mgumu kuliko uliopita," alisema kocha huyo raia wa Argentina.

Kocha huyo amesema ingawa yeye na baadhi ya mashabiki wangependa washinde mabao mengi, lakini haitokuwa rahisi kutokana na wapinzani walivyojipanga, lakini pia wachezaji wake wanavyopoteza nafasi.

"Yanga tunaingia zaidi ya mara 20 kwenye eneo la hatari la mpinzani wetu, lakini tumekuwa tukikosa sana," alisema kocha huyo.


Kocha Mkuu wa KMC, Abdihamid Moallin, amesema ni ngumu sana kucheza na timu kama Yanga, hivyo amewataka wachezaji wake kuwa makini na kutofanya makosa mara kwa mara.

"Unabidi tucheze mchezo huu kwa umakini mkubwa, nafikiri vijana wako tayari, nafikiri Yanga imebadilika siyo kama ile ya msimu uliopita," alisema kocha huyo raia wa Somalia.

Aliwataka wachezaji wake wasifanye makosa kama waliyofanya dhidi ya Azam FC, Septemba 19 na kujikuta wakibugizwa nyumbani, mabao 4-0.



Michezo
Jumapili Septemba 29, 2024
Nipashe



Solskjaer: Utd ilifanya makosa kumrejesha Ronaldo UK. 21

# YANGA VITANI DAR, SIMBA SC DODOMA



Mchezaji wa timu ya mpira wa kikapu ya Polisi, akimiliki mpira huku akizongwa na wachezaji wa Anmacha, wakati wa mchezo wa michuano ya JMK Park inayofanyika katika viwanja wa Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

●●● Ni mechi za Ligi Kuu Tanzania bara, kila mmoja akijinadi kuwa....

**Na Adam Fungamwango**

WAKONGWE wa soka la Tanzania, Simba na Yanga, leo watakuwa kwenye majiji tofauti kucheza michezo yao ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

**Wakati Simba watakuwa Makao Makuu ya nchi, kucheza na wenyeji Dodoma Jiji, kwenye Uwanja wa Jamhuri, saa 12:30 jioni, Mabingwa Watetezi, Yanga wao watakuwa jijini Dar es Salaam kucheza dhidi ya KMC,pambano linalotarajiwa kuanza saa 3:00 usiku, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi.**

Utakuwa ni mchezo wa nne kwa Simba katika Ligi Kuu na wa tatu kwa Yanga kwa kuwa zilikuwa kwenye shughuli pevu ya kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa na sasa zimerejea.

Simba itaingia uwanjani hapo ikiwa na kumbukumbu katika mchezo wa mzunguko wa pili wa Ligi Kuu msimu uliopita, uliopigwa Mei 17 mwaka huu, ikipata ushindi wa bao 1-0 lililowekwa wavuni na Freddy Michael ambaye aliachwa mwishoni mwa msimu huo.

Yanga ina kumbukumbu nzuri ya kutoa kipigo cha mabao 5-0 dhidi ya KMC kwenye uwanja huo huo, Agosti 23 mwaka jana, ikiwa ni mchezo mzunguko wa kwanza wa ligi ya msimu uliopita.

Kocha wa Simba, Fadlu Davis, amesema itakuwa ni mechi ngumu kama zingine zote, huku akisikitika kuwakosa nyota wake ambao ni Joshua Mutale, Yusuph Kagoma na Mzamiru Yassin.

Hata hivyo, Mzamiru hajaonekana katika michezo mbalimbali ya hivi karibuni.

"Itakuwa mechi ngumu kama nyingine tu zilivyokuwa, nimejaribu kufuatilia, lakini hakuna mfumo halisi ambao tutakwenda kucheza na wala walionao wapinzani wetu, tunakwenda kucheza kujaribu kupata pointi tatu.

Ninachotaka kusema ni kuwataka tu mashabiki wa Simba waliopo Dodoma

INAENDELEA UK 23

# Mbeya City yainyoa Mbeya Kwanza, Mtibwa ikizidi kutakata championship

**Na Mwandishi Wetu**

BAO pekee la David Mwasa, juzi, liliiwezesha Mbeya City kuondoka na ushindi wa bao 1-0, katika mchezo wa raundi ya pili ya Ligi ya Championship dhidi ya Mbeya Kwanza, kwenye uwanja wa Sokoine Jijini Mbeya.

Ulikuwa mchezo mkali wa dabi ya Mbeya, kila timu ikitaka kudhihirisha kuwa ndiyo mbabe wa jijini hilo, lakini bao la nahodha huyo wa zamani wa Mbao FC, liliamua matokeo.

Hii ni mechi ya kwanza kwa Mbeya City kupata ushindi kwenye ligi hiyo, baada ya kulazimishwa sare ya mabao 2-2 wiki iliyopita dhidi ya Bigman FC, ambayo zamani ilitwa Mwadui FC.

Kinakuwa kichapo cha pili kwa Mbeya Kwanza kwani mchezo wao wa raundi ya kwanza walipata kipigo cha mabao 2-1 dhidi ya Songea United, Uwanja wa Majimaji, Ruvuma.

Kwenye Uwanja wa Jamhuri Morogoro, timu ya Mtibwa Sugar imeonekana haishikiki kwenye ligi hiyo, baada ya kupata ushindi wake wa pili mfululizo, ikiitwanga Cosmopolitan, mabao 2-0.

Mabao ya Mtibwa ambayo ilishuka daraja kutoka Ligi Kuu msimu uliopita, yaliwekwa wavuni na Omari Marungu, dakika ya tano ya mchezo, na Raizin Hafidh dakika ya 35.

Linakuwa ni bao la tatu kwa mchezaji huyo kwa michezo miwili tu ya Ligi ya Championship aliyocheza, kwani katika mechi ya ufunguzi wiki iliyopita, mabao mawili, Uwanja wa Manungu Complex, Turuani, Morogoro na kuipa ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Green Warriors.

Timu ya Stand United, ikiwa nyumbani, Uwanja wa Kambagare Shinyanga, imepata ushindi wa bao 1-0, likiwekwa wavuni na Andrew William.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >